# Nipashe

Ijumaa Julai 3, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580274

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Mwalimu atiwa korokoroni kwa tuhuma za kumtapeli mwenzake

UKURASA 16

# Faida, hasara Tanzania kuingia uchumi wa kati

**SERIKALI** yaanika mambo 10 yaliyoibeba, wachambuzi wabainisha yatakayotokea...*Endelea ukurasa 2 & 11*



Wanafunzi wakigombea kupanda daladala katika kituo cha Kitunda, jijini Dar es Salaam jana, basi moja limeruhusiwa kuchukua wanne pekee. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## COVID-19

'Usichukulie poa unategemewa'

- **Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka**
- **Kaa kwa kuachi-ana nafasi hatua 2 au 3**
- **Vaa barakoa**
- **Ukikohoa au ku-piga chafya ziba mdomo**

## WADAIWA KUMUUA KAKA KISA MIRATHI

UKURASA 3

# ZEC yafyeka majimbo ya uchaguzi Zanzibar

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


**MICHEZO** SIMBA YAFURAHI KUIFUATA YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6




Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu mambo mbalimbali ikiwa pamoja na sababu zilizoifanya Tanzania kutangazwa na Benki ya Dunia kuwa imeingia katika orodha ya nchi zenye uchumi wa kati. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Faida, hasara Tanzania kuingia uchumi wa kati

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI serikali ikitaja mambo 10 yaliyochangia Tanzania kuingia katika kipato cha kati kwa kundi la chini mwaka 2020, wataalamu wa uchumi wameeleza faida na hasara za kuingia kwenye orodha hiyo.

Juzi, Benki ya Dunia ilitangaza Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zilizofikia uchumi wa kati kwa kundi hilo ikiwa ni miaka mitano kabla ya lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 iliyoandaliwa mwaka 1999.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alisema Tanzania ilipaswa kufikia hatua hiyo miaka mitano ijayo.

Alifafanua kuwa katika Benki hiyo kuna mgawanyo wa makundi matatu kulingana na viwango vyao vya uchumi na Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu pekee za Afrika zilizoingia kwenye kundi la kipato cha kati juzi na imekuwa nchi ya pili kwa Afrika Mashariki.

"Hatua hii imeakisi azma ya Rais John Magufuli ya kuwa sisi si nchi maskini, uchumi wa kati unamaanisha nchi imetoka katika umaskini na kuwa matajiri, lakini siyo sana," alisema.

Dk. Abbasi aliyataja mambo 10 yaliyoibeba Tanzania kuwa ni pamoja na kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati na kufanya uamuzi mgumu.

Mengine ni Amani na utulivu, mipango thabiti ya maendeleo, utekelezaji usioyumba, azma ya kujitegemea, nidhamu katika matumizi, kuimarisha miiko ya viongozi, kuwekeza katika maendeleo ya watu na sekta binafsi yenye tija.

Alibainisha kuwa dira inakazia kuwa, ili kufikia uchumi wa kati, ni lazima kuwa na uchumi imara na uchumi wa kipato cha kati uwe umewekezwa kwenye viwanda jambo ambalo limefanyika na kwa kipindi cha miaka mitano, vipo zaidi ya 8,000 vilivyoanzishwa, kujengwa na vingine vinamaliziwa.

Dk. Abbasi alisema viongozi wa serikali za awamu zote wamechangia kufikia hatua hiyo, akisisitiza kuwa uwekezaji katika miradi ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa, imechangia kwa kiwango kikubwa.

"Kama kuna kitu kimechagiza sana ni uamuzi wa serikali wa kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati, leo Tanzania inatekeleza miradi ambayo wengine wananuna, viwanda vimejengwa," alisema.

Alisema kuna wakati serikali zote zimefanya uamuzi mgumu hadi kusababisha kutungiwa majina ikiwamo udikteta.

**FAIDA NA HASARA**

Wakati serikali ikiyasema hayo, watalaamu wa uchumi wamebainisha faida na hasara kwa Tanzania kuingia katika uchumi huo.

Katika mazungumzo na Nipashe jana, mchumi Junior Ndesanjo alisema dhana ya nchi kuingia katika uchumi wa kati ina maana kwamba pato la mwananchi limekua na thamani ya bidhaa kwenye masoko imeongezeka.

"Uchumi wa kati juu (kipato cha mwananchi) ni Dola za Marekani 4,000 na uchumi wa kati chini ambayo Tanzania tumeingia humo ni kuanzia Dola 1,036 (Sh. milioni mbili) kwa mwaka, siyo kila Mtanzania anapato hilo, bali ni pato la wastani," alifafanua.

Ndesanjo alisema uchumi wa kati wa chini unalitambulisha taifa kimataifa, hivyo kuwa na uwezekano mkubwa wa kupata wawekezaji wengi.

"Wawekezaji wengi wanaenda Kenya ambayo ilipanda tangu mwaka 2015 kuliko Tanzania, tutarajie wawekezaji wengi zaidi," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini (Repoa), Dk. Donald Mmari, alisema tafsiri ya hatua hiyo ni kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta mbalimbali.

Alisema inaonyesha Pato la Taifa limeongezeka kiasi kwamba likigawanywa kwa vigezo vinavyotumika, linaiondoa Tanzania katika orodha ya nchi maskini.

"Eneo la ardhi linalolimwa limeongezeka, na uzalishaji wa mazao umeongezeka sana, sekta ya uchukuzi unaona kuna ubebabaji wa mizigo umeongezeka, sekta ya ujenzi nyumba zinajengwa na majengo mengi sana," alibainisha.

Dk. Mmari alisema sekta ya utalii pia imeongezeka kwa idadi ya watalii kufikia zaidi ya milioni 1.5 tofauti na miaka 20 iliyopita walipokuwa 50,000 kwa mwaka.

Alisema kaya zilizounganishwa na umeme na maji zimeongezeka na wananchi wanaomiliki mali mfano pikipiki ambazo kwa sasa vijana wengi wanamudu kununua. Pia kaya zinamiliki redio, luninga na dhana za kisasa za kilimo.

Mtaalamu huyo pia alisema nyumba za bati zimeongezeka kwa sasa, tofauti na miaka 20 iliyopita ambapo nyumba nyingi ziliezekwa kwa nyasi.

"Kuna uwezekano wa mikopo nafuu kupungua kwa kuwa unapofikia pato la kati la chini, kuna misaada ulikuwa unapewa kama mikopo ambayo mingi iliangalia hatua za uchumi, utaiokosa.

"Kenya riba yao ni kubwa kidogo. Nchi maskini zinaonewa huruma kwa sababu ya pato lao. Kama mkopo riba ni asilimia 15, nchi maskini inapewa asilimia 10, kwa hatua hii tutaingia kwenye riba kubwa," alisema.

Alisema pia fedha za misaada ambayo Tanzania ilipaswa kuzipata bure, itazikosa kwa sababu imekua kiuchumi.

Alisema kuwa, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, kunahitajika jitihada za zaida kuendana na ongezeko la watu, kinyume chake uchumi utasuasua.

***Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA) na Salome Kitomari (DAR)**

## ZEC yafyeka majimbo ya uchaguzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imefanya mapitio ya idadi, majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi Zanzibar na kuyapunguza kutoka 54 hadi 50.

Imesema mapitio hayo yamefanyika kwa kuzingatia kifungu cha 120(4) cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa ZEC, Jaji Hamid Mahmoud, alisema tume imeamua kuyafuta majimbo manne ya uchaguzi, hivyo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kutakuwa na 50 badala ya 54 yaliotumika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Jaji Mahmoud alisema kuwa katika uchaguzi uliopita, majimbo ya uchaguzi yalikuwa 54, lakini kuliibuka malalamiko ya wadau kuhusu mabadiliko yaliyofanyika kupata idadi hiyo ya majimbo kutokana na kusababisha usumbufu kwa wapigakura kwa baadhi ya majimbo.

Kiongozi huyo alisema wadau wa uchaguzi waliibua matatizo ya uwapo wa tofauti kubwa ya wapigakura kati ya jimbo moja na lingine.

Alisema kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, ZEC ilijadili kwa kina suala hilo na iliamua kwa mamlaka iliyonayo kufanya uchunguzi wa kina juu ya madai ya dosari ziliripotiwa na wadau kwa lengo la kujiridhisha kama kweli kuna shida.

"Katika kazi hiyo, tume iliangalia kigezo cha idadi ya watu katika majimbo na uwakilishi unaofaa katika miji mikubwa na miji ya mashamba yenye idadi ndogo ya watu," alisema.

Alibainisha kuwa tume imeangalia kigezo cha ongezeko la idadi ya watu katika maeneo mbalimbali kwa kutumia takwimu za hesabu ya Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.

Mwenyekiti huyo alisema uchunguzi huo unaonyesha idadi ya watu wanaohamia katika miji ya mashamba kutokana na sababu mbalimbali za kiuchumi na kijamii, inaongezeka kwa kasi sana katika maeneo ya Wilaya za Magharib A na B Unguja, Wete na Mkoani, Chakechake kisiwani Pemba.

Alisema tume pia iliangalia kigezo cha njia kuu za usafiri katika majimbo na mipaka ya utawala ili kuondoa usumbufu wa kuwachanganya wananchi katika maeneo yao ya uchaguzi.

Aliyataja majimbo yaliyofutwa kuwa ni Jimbo la Kiwengwa, Mtopepo, Kijitoupele na Chukwani ambapo Wilaya ya Magharibi B kutakuwa na majimbo matano badala ya saba na Kaskazini B kutakuwa na majimbo matatu badala ya manne na Magharib A kutakuwa na majimbo matano badala ya sita.

Alisema kwa upande wa Pemba, Jimbo la Mgogoni limefutwa na limeundwa Jimbo la Pandani, hivyo Unguja sasa kutakuwa na majimbo 32 na Pemba 18.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Kippi Warioba, akinawa mikono ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa vizimba sita vya maji ya kunawa, vilivyotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkatika soko la Mbuyuni, Manispaa ya Moshi, jana. **PICHA: JAMES LANKA**

# Watuhumiwa kumuua mdogo wao wakigombania nyumba

**Na Romana Mallya**

NDUGU wawili wa familia moja wanadaiwa kumuua mdogo wao, Mandela Malisa, kwa madai ya kumkuta amelala chumba cha baba yao mzazi ambaye kwa sasa ni marehemu, chanzo kikidaiwa kugombania nyumba ya urithi.

Tukio hilo lilitokea juzi Kata ya Sinoni, mkoani Arusha baada ya ndugu hao ambao ni dada wa marehemu kumshambulia ndugu yao na kitu cha ncha kali na kufariki dunia alipofikishwa hospitali. Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Salum Hamduni, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema bado halijamfikia ofisini kwake.

Baba mkubwa wa marehemu, Emrod Malisa, alidai kabla ya tukio hilo, kijana aliyeuawa alimweleza kuwa amekosana na dada zake.

"Nilimwambia (marehemu) apumzike ili jioni (siku moja kabla ya mauaji hayo) niwaite dada zake, saa nane dada zake wakaja wenyewe kabla ya kuwaita, walikuja kushtaki kuwa wamekosana na ndugu yao." "Niliwaambia siwezi kusikiliza mashtaka ya upande mmoja nitawakutanisha siku ya Jumapili asubuhi (kesho kutwa) ili tuongelee hayo mambo tukaagana wakaondoka."

Malisa alisema jana asubuhi alijulishwa kuhusu msiba huo na alipouliza chanzo akaambiwa kulitokea ugomvi baada ya Mandela kuhama kutoka chumba alichokuwa anakaa na kuhamia cha baba yake mzazi.

"Hawa dada zake wanasema hicho chumba kisiingiliwe na mtu, hii ni nyumba ya familia, hapa baba alikuwa na mke wa kwanza ana watoto wakubwa na akaoa mwingine, akazaa watoto wengine."

"Baba yao alisema nyumba ni ya familia na kwa sababu aliacha mtoto mdogo hawa wakubwa wa kike wakae wapumzike mpaka watakapoolewa."

Naye, Balozi wa Mtaa wa Onjavutiani, Kata ya Sinoni, Arusha, Praygod Mhando, alisema alipigiwa simu na kuelezwa Mandela ameshambuliwa na ndugu zake wawili nyumbani na baadaye alipelekwa hospitali kwa matibabu na kufariki dunia.

"Tulikwenda polisi na majirani wawili kutoa taarifa na polisi walikwenda eneo la tukio, walioshuhudia tukio hilo walisema kwamba walikuwa na ugomvi wa kifamilia kwa sababu ya nyumba ya baba yao walikuwa wakigombania," alisema.

Alisema msiba wa mwisho ambao ulifanyika hapo nyumbani ulikuwa ni wa mama yao na kwamba waliumaliza vizuri bila tatizo na kama mtaa hawakujua kama kulikuwa na matatizo mengine kwenye familia hiyo.

"Mandela alikuwa amelala chumbani ndugu zake wa kike wakaja wakamwambia kwanini unalala kwenye chumba cha baba wakati hujaruhusiwa kulala humo, ndipo ugomvi ulipoanza," alisema.

# Taasisi za Wizara ya Mambo ya Nje zatakiwa kujitegemea

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imezitaka Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kufanya kazi kwa ubunifu na kufanya uwekezaji wenye tija.

Imesema lengo ni kuhakikisha zinajiendesha zenyewe na kuipunguzia Serikali kuu mzigo.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Brigedia Jenerali, Wilbert Ibuge, alipofanya ziara katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji yanayomilikiwa na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) na kuwataka watendaji wake kuwa wabunifu. Aliwataka taasisi hizo kuhakikisha zinajiendesha kwa ubunifu na kuondokana na dhana kuwa Serikali itazisaidia kujiendesha kwa kisingizio cha uwapo wa janga la corona.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa kituo hicho, Elishilia Kaaya, alisema taasisi hiyo imeyapokea maagizo hayo ya serikali na kwamba changamoto kubwa iliyopo mbele yao licha ya kuathirika na janga la corona ni kuhakikisha kwamba inajiendesha bila ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

# Ajali magari manne yaua, yafunga barabara Dar-Moro

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MTU mmoja amefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa katika ajali iliyotokea usiku wa kuamkia jana katika eneo la Mkaramo, Mlandizi wilayani Kibaha, Pwani.

Ajali hiyo ambayo ilisababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara ya Dar es Salaam-Morogoro kwa kuwa na foleni kwa zaidi ya saa sita, ilihusisha magari manne.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Julai Mosi majira ya saa tano usiku huko Mlandizi baada ya gari lenye namba za usajili T 597 CBC aina ya Fuso likiwa na shehena ya viazi mviringo, kugongana na gari namba T 376 BTH/ T 822 BQA aina ya Howo, mali ya kampuni ya usafirishaji ya Safari Cargo likiwa na shehena ya mafuta dizeli likitokea Dar es Salaam kwenda Rwanda.

Alisema kuwa baada ya ajali hiyo, magari mengine mawili yaliyokuwa yanafuata nyuma ya gari la mafuta, yaligongana.

Kamanda Wankyo alisema magari hayo ni T 386 DRQ / T.387 DRQ aina ya Scania lililokuwa limebeba shehena ya saruji likitokea Dar es Salaam kwenda Dodoma na T.225 DCV/ T 839 ABK aina ya Howo likisafirisha dizeli kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro, mali ya Kampuni ya Continenta.

Alisema kuwa kufuatia ajali hiyo, magari yaliyokuwa yakisafirisha mafuta yaliungua moto, huku kukitokea uharibifu wa barabara kwenye eneo la ajali.

Kamanda Wankyo alimtaja aliyefariki katika ajali hiyo kuwa ni Rahim Kulwa, aliyekuwa dereva wa gari namba T 225 DCV/T839 ABK na majeruhi Omary Rayi, Mfaume Damson na Habibu Omary.

Alisema mwili wa Kulwa umehifadhiwa katika Hospitali ya Tumbi na majeruhi walikuwa wanaendelea na matibabu.

IN LOVING MEMORY
OF LATE CRISPIN S.E. MWANYIKA



***"Come to me, all you who are weary and burdened, and I will give you rest. Take my yoke upon you and learn from me, for I am gentle and humble in heart, and you will find rest for your souls. For my yoke is easy and my burden is light." Matthew 11:28-30***

On 2nd JULY 1999, YOU WERE CALLED TO GO AND BE WITH OUR LORD.
IT IS NOW 21 YEARS WE HAVE LIVED WITHOUT YOUR LOVING CARE.

YOU ARE FOREVER MISSED BY YOUR WIFE JANE, YOUR CHILDREN NANCY, ENG.GEOFFREY, DR. MARY, DAVID, GRAND CHILDREN, YOUR IN-LAWS, BROTHERS & SISTERS, RELATIVES & FRIENDS.

**THERE WILL BE A REQUIEM MASS AT ST MARTHA ROMAN CATHOLIC CHURCH, MIKOCHENI B ON SUNDAY 5.07.2020 AT 9.00AM.**

**OUR PRAYER IS ALWAYS FOR YOUR SOUL TO REST IN ETERNAL PEACE TILL WE MEET AGAIN AMEN.**

# Meneja Bandari mbaroni tuhuma kupokea rushwa

**Na Fatma Mtutuma, UDOM**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imemkatama aliyekuwa Meneja wa Bandari ya Kipumbwi, Steven Mbakweni, kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa Tanga, Anthony Gang'olo, alisema Mbakweni aliomba rushwa ya Sh. 900,000 kwa mteja wake kwa ajili ya kumruhusu asafirishe mzigo kutoka Pangani kwenda Zanzibar.

"Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba Mbakweni aliomba na alishawishi hongo baada ya mteja wake kumpatia nyaraka zote zilizotolewa na ofisi ya Bandari baada ya kufanya malipo ili kusafirisha mzigo wake katika bandari hiyo," alifafanua Gang'olo.

Aliongeza kuwa: "Nyaraka hizo zilikataliwa na Mbakweni kwa madai kwamba hazitambui akiwa na lengo la kushawishi apewe hongo ya Sh. 900,000 kwa ajili ya kusafirisha mzigo huo."

Gang'olo alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa baada ya kupokea rushwa ya Sh. 270,000 kama mtego baada ya mteja huyo kuomba apunguziwe.

"Mtuhumiwa alikamatwa katika bandari ya Kipumbwi majira ya saa 9:00 alasiri akiwa amepokea rushwa ya Sh. 270,000 baada ya mteja kubembeleza apunguziwe,"alisema Gang'olo.

Mkuu huyo alitoa onyo kwa watumishi wa umma wenye tabia hizi hususani katika kipindi hiki cha uchaguzi kuwa kitendo hiko ni kosa chini ya kifungu cha 15 cha kupambna na kuzuia rushwa.

# Serikali yafuta vipindi vya nyongeza

**Fatma Mtutuma na Mary Mshami, UDOM**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imefuta saa mbili za nyongeza za masomo zilizokuwa zinafundishwa kila siku kwa shule za msingi na sekondari.

Saa hizo ziliongezwa kufidia muda uliopotea kutokana na wanafunzi kuwa nyumbani tangu Machi 18, mwaka huu, kutokana na janga la corona. Shule zilifunguliwa Jumatatu wiki hii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Kamishina wa Elimu, Lyabwene Mtahabwa, kwa sasa wanafunzi watarejea kwenye utaratibu wa kusoma vipindi nane kwa siku.

Alisema tathmini iliyofanyika ya utekelezaji wa malekezo ya awali ya Wizara, imeridhika kuwa kuongezeka kwa saa mbili kila siku ni vigumu kutekeleza.

"Hii ni kutokana na kuwepo kwa shule ambazo kwa sababu mbalimbali zimepewa vibali vya kuendesha masomo kwa mfumo wa 'double shift',"alifafanua Mtahabwa.

Aliongeza: "Na kutokana na tatizo la usafiri kwa wanafunzi wanaoishi mbali na shule wanazosoma, Wizara inaelekeza shule zirejee kwenye ratiba zao za kawaida za vipindi nane kwa siku."

Aidha, alisema iwapo uongozi wa shule utaona kuna sababu za msingi za kuongeza muda wa taaluma basi zitumike muda uliopangwa kwenye ratiba ya shule kwa ajili ya kutekeleza mtaala wa ziada au shughuli za nje ya darasa.

Juni 17, mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, alitangaza mabadiliko ya ratiba za masomo katika shule za msingi na sekondari kwa kuongeza saa mbili kila siku kwa ajili ya kufidia muda uliopotea kutokana na mapumziko ya corona.




Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. David Mwamfupe (kulia), akipokea msaada wa vifaranga vya kuku wa nyama vyenye thamani ya Sh. milioni 3 kutoka kwa Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Felix Nandonde, kwa ajili ya vikundi vya vijana jijini hapo jana. Wengine ni Ofisa Mifugo wa Jiji la Dodoma, Dk. Gratian Mwesiga (wa pili kushoto) na Mkuu wa Idara Maendeleo ya Jamii wa Jiji hilo, Sharifa Nabalang'anya. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TCRA yafafanua umiliki laini moja

**Faudhia Sultan na Magdalena Haule, UDOM**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetoa ufafanuzi wa urasimishaji umiliki laini za simu zaidi ya moja katika mtandao mmoja.

Ufafanuzi huo umetolewa baada ya kuanza rasmi utekelezaji wa kanuni za umiliki wa laini ulioanza Julai mosi, mwaka huu.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwenye gazeti hili na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, mtu binafsi anatakiwa kumiliki laini moja kwa ajili ya kupiga simu za sauti, kutuma ujumbe mfupi pamoja na matumizi ya data.

Vile vile, idadi ya laini zisizodhidi nne kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa matumizi ya mawasiliano kati ya mashine na mashine.

Tangazo hilo lilibainisha kuwa kwa kampuni au taasisi idadi ya laini zisizozidi 30 kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa ajili ya kupiga simu za sauti, kutuma ujumbe mfupi pamoja na matumizi yake.

Pia, idadi ya laini isiyozidi 50 kwa kila mtoa huduma za mawasiliano kwa matumizi ya mawasiliano kati ya mashine na mashine.

Laini zilizosajiliwa kwa matumizi yaliyoainisha kwenye kanuni, hazipaswi kutumiwa kwa kubadilishana, na kwamba wanaweza kuruhusiwa kusajili na kumiliki laini zaidi zilizoainishwa kwa kuomba na kupata idhini kutoka TRCA.

Mamlaka hiyo ilifafanua kuwa, yeyote atakayekiuka masharti ya kanuni hizo atakuwa ametenda kosa la jinai.

"Utaratibu wa kuomba idhini ya umiliki wa laini za simu zaidi ya moja katika mtandao mmoja unaendelea," alisema.

Kadhalika Julai 31, mwaka huu, utakuwa mwisho kwa wanaomiliki laini zaidi ya moja katika mtandao mmoja.

"Utaratibu wa kuomba idhini ya kumiliki laini mpya za ziada katika mtandao mmoja unaendelea na mteja anaweza kupata huduma kupitia wakala au kwenye ofisi za watoa huduma, kwa njia za kielektroniki, mtoa huduma atawasilisha maombi ya mteja wake," ilifafanuliwa.

## HABARI KITAIFA




Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa tatu kushoto), akishiriki uzinduzi wa huduma ya CRDB Malkia. Wengine ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'I Issa (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), Ofisa Mkuu wa Biashara Dk. Joseph Witts, Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Neema Mori na Ofisa Mkuu wa Fedha, Fredrick Nshekanabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Spika aipongeza CRDB riba nafuu mikopo wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ameipongeza Benki ya CRDB kwa kupunguza riba kwa mikopo ya wanawake wajasiriamali.

Mikopo hiyo inapatikana kupitia huduma ya "CRDB Malkia" hadi kufikia asilimia 14 kwa mwaka.

Akizungumza katika uzinduzi wa CRDB Malkia, Dk. Tulia alisema hatua ya benki hiyo kupunguza riba kwa asilimia 10 kutoka asilimia 24 iliyokuwa ikitozwa mwanzo, itasaidia wanawake wengi zaidi kuchangamkia fursa ya mikopo hiyo. "Kupungua kwa riba ina maana inapunguza mzigo mkubwa wa marejesho kwa wanawake na kuwafanya kuwa na fedha nyingi kwa ajili ya uwekezaji katika biashara zao, hivyo kupelekea kufanikisha zaidi," alisema Dk. Tulia.

Aisema pamoja na utafiti kuonyesha wanawake wamekuwa na ushiriki mkubwa katika shughuli za uchumi nchini, kwa asilimia 54, ni asilimia 60 tu ya wanawake ndio wenye kufikiwa na huduma rasmi za kifedha.

"Niwapongeze pia kwa kuboresha masharti ya dhamana ili kutoa fursa kwa wanawake wengi zaidi kuweka mikopo," aliongezea Dk. Tulia, huku akiwataka wanawake pia wajitokeze kwa wingi kufungua akaunti ya Malkia itakayosaidia kufanikisha malengo yao kwa kujiwekea akiba kidogokidogo, jambo litakalosaidia kujenga imani kwa taasisi za fedha.

"Mimi ni mmoja wa wanawake waliofungua akaunti ya Malkia wakati ikianzishwa mwaka 2009, nimefurahi kuona leo hii Benki yetu ya CRDB ikifanya maboresho yatakayoweza kumkomboa mwanamke."

Dk. Tulia alisema jitihada hizi zinazofanywa na Benki ya CRDB katika uwezeshaji wa makundi mbalimbali ya wananchi zimekuwa na msaada mkubwa katika kuisaidia Tanzania kufikia lengo la kuwa nchi yenye uchumi wa kati.

"Nimefurahi kuona leo hii tukiwa tunajivunia kuwa nchi ya uchumi wa kati, Benki yetu ya CRDB inaendelea kutubeba wanawake na kuwezesha kufikia malengo yetu ya nchi na dunia katika kuwa na usawa katika ushiriki katika shughuli za maendeleo kama ilivyoainishwa katika mpango wa Maendeleo Endelevu 2030 wa Umoja wa Mataifa," alisema Dk. Tulia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema huduma ya CRDB Malkia imelenga katika kumtambua, kumpa nafasi na kumwezesha mwanamke wa Kitanzania kufikia malengo yake kupitia mikopo ya biashara na ujasiriamali, kujiwekea akiba kwa akaunti ya Malkia na mafunzo ya uendeshaji biashara.

"Mpaka kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, benki yetu tayari ilikuwa imeshatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 600 kwa wanawake zaidi ya 55,000," alisema Nsekela huku akibainisha kuwa zaidi ya wanawake 30,000 wameshajiunga na akaunti ya Malkia.

## Makasisi kortini kwa tuhuma za kuishi bila vibali

**Na Hellen Mwango**

WACHUNGAJI wawili Raia wa Congo, Patient Sunga (53) na Michou Sunga(50) wa kanisa la Mlima wa Moto Buza, Temeke jijini Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakikabiliwa na shtaka la kuishi nchini bila kibali.

Makasisi hao walisomewa mashtaka yao jana katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabati.

Mwendesha Mashtaka wa Idara ya Uhamiaji, Godfrey Ngwijo, alidai kuwa Mei 3, 2019 Ilala, jijini Dar es Salaam, wakiwa raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, wamekuwa wakiishi nchini bila kibali.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao ambao ni mume na mke, wamekuwa wakiendesha shughuli zao katika Kanisa la Mlimawamoto, Buza Wilaya ya Temeke.

Washtakiwa hao walikiri mashtaka yao baada ya kusomewa.

# TNBC kufanyia kazi soko mazao ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC) kupitia kikosi kazi chake cha kilimo kimekutana kujadili namna bora ya kukuza soko la ndani na nje la mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji kwa kumnufaisha mkulima na kutoa mchango stahiki katika kukuza uchumi wa taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha kikosi kazi hicho jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Gerald Kusaya, alisema wajumbe walijadili pia umuhimu wa kuyaongezea thamani mazao ili kupata soko la uhakika la ndani na nje ya nchini.

"Katika kutekeleza azma ya serikali ya awamu ya tatu ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025, kama wasimamiaji wa sekta ya kilimo ni lazima kuhakikisha tunakutana na wadau wa sekta binafsi na kuweka mazingira mazuri yatakayoleta mageuzi katika sekta hii," alisema Kusanya.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi yatakayowahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji pamoja na kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta ya kilimo.

"Kumekuwapo na changamoto za uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna, kukosekana kwa mbegu bora na viwatilifu. Kikosi kazi cha kilimo kimeazimia kuondokana na changamoto hizo ili kuongeza thamani ya mazao na kuleta tija zaidi kwa wakulima," alieleza.

Aliongeza kuwa serikali imeweka mazingira kwa wananchi kukopa fedha zinazopelekwa kwenye halmashauri kwa vikundi vya kinamama na vijana ili kuchangia ukuaji wa sekta ya kilimo hapa nchini.

"Serikali imekuwa ikipeleka fedha katika halmashauri zote nchini ambazo wananchi wanaweza kukopa kupitia vikundi vya kijamii na kuwekeza katika shughuli za maendeleo ikiwamo sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Tunaamini kwa hatua hizo zinazochukuliwa na serikali, itachochea hamasa kwa wananchi kutumia mikopo hiyo kujinufaisha kiuchumi," alieleza. Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema baraza litaendelea kuunganisha wadau wa sekta binafsi na serikali ili kujenga uchumi jumuishi na wezeshi hali ambayo italeta maendeleo kwa haraka nchini.

"Serikali imechukua hatua kadhaa ikiwamo kujenga miundombinu ambayo itahisishaji usafirishaji wa pembejeo kufika maeneo husika, lakini itasaidia usafirishaji wa mazao katika masoko ya ndani na nje," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Godfrey Malekano, alisema TMX itaendelea kuhakikisha bidhaa za kilimo zinapata

masoko ya uhakika ili kuendelea kuwanufaisha wakulima hapa nchini. "TMX tutaendelea kuweka mazingira mazuri na uwazi katika mchakato wa ununuzi wa mazao kwa lengo la kuhakikisha wakulima wanapata thamani halisi ya uwekezaji wao," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ulinzi wa uhakika maeneo ya madini nchini muhimu

**TUKIO** la ujambazi lililotokea mapema wiki hii katika kiwanda cha uchenjuaji wa madini ya dhahabu wilayani Kahama mkoani Shinyanga na kuuawa watu wanne, kimetuachia funzo kuwa maeneo ya madini yanahitaji ulinzi wa uhakika.

Katika tukio hilo, wafanyakazi wanne wa kiwanda hicho cha uchenjuaji wa dhahabu kwenye mgodi mdogo wa Ntambalale, kijiji cha Wisolele, wilayani Kahama, waliuawa kwa kucharangwa na mapanga na watu wasiojulikana kisha kutokomea.

Kwa mujinu wa uongozi wa mgodi huo, tukio hilo lilitokea majira ya saa tisa usiku, ambapo wafanyakazi watano wa kiwanda hicho, walivamiwa na kucharangwa mapanga na watu wasiojulikana na kuibiwa kaboni, huku wanne kati ya hao wakipoteza maisha papo hapo na mmoja, akijeruhiwa.

Tukio hilo limeelezwa kuwa ni mwendelezo wa matukio ya uhalifu kwani mwanzo wa mwezi uliopita pia kulitokea uvamizi kwenye kiwanda cha uchenjauji wa madini na kuiba kaboni, lakini hakuna mtu aliyejeruhiwa.

Matukio ya uhalifu husussan ujambazi yanaweza kutokea mahali popote, lakini tunaona kuwa kutokana na kujirudia katika maeneo yenye madini ni tishio kwa usalama wa madini na wamiliki wa migodi au viwanda vya kuyachenjua.

Tunasema hivyo kutokana na thamani ya madini na kuthamini mchango wake katika uchumi wa nchi yetu.

Ikumbukwe kuwa kwa sasa sekta ya madini ni miongoni mwa sekta zinazokuwa kwa kasi, ikiwamo kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Kwa mfano, mwaka 2019, uchumbaji wa madini na mawe ulishika nafasi ya kwanza katika ukuaji wa kasi kwa asilimia asilimia 17.7.

Kasi ya ukuaji huo imetokana na jitihada zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na Rais John Magufuli, baada ya kubaini kuwa sekta ya madini ikisimamiwa inaweza kuiwezesha Tanzania isonge mbele kiuchumi.

Katika kusimamia rasilimali hiyo na kuhakikisha inawanufaisha Watanzania na kuondokana na umaskini, ni lazima kuwapo kwa ulinzi wa kutosha kwa ajili ya usalama wa madini na, wachimbaji, wawekezaji na wafanyakazi katika migodi na viwanda vya uchenjuaji.

Kuwapo kwa usalama kunasaidia kuepusha wizi na utoroshaji wa rasilimali hiyo, ambao katika miaka ya nyuma ulikuwa imeshamiri na kuifanya nchi yetu kuwa shamba la bibi.

Hata hivyo, hatua zilizochukuliwa na Rais John Magufuli ya kufuatilia madini kwa karibu kuanzia uchimbaji migodini hadi mauzo pamoja na usalama ikiwamo ujenzi wa ukuta huko Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara katika machimbo ya tanzanite, zimeleta mabadiliko na kuinufaisha nchi.

Pamoja na ukuaji wa kasi na mchango wa sekta ya madini kwa uchumi wa nchi yetu, tunaona kuna umuhimu wa serikali kuchukua hatua za dhati kuhakikisha kuwa maeneo ya migodi na viwanda vya uchenjuaji wa madini yanakuwa na usalama wa uhakika ili kuepusha matukio ua uhalifu unaoweza kutishia maisha ya watu na madini.

Kwa kuwa wahalifu husussan majambazi wanajua kuwa madini yana thamani kubwa, ndio maana wanatumia nguvu kubwa kuvamia migodi kwa lengo la kuyaiba.

Ulinzi wa uhakika hauhitajiki kwenye migodi mikubwa pekee, bali hata katika machimbo ya wachimbaji wadogo.

Tunaamini kuwa Jeshi la Polisi litaweka utaratibu wa kuilinda migodi yote, ili shughuli za uchimbaju zifanyike katika mazingira salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# RC Malima na staili yake kuinua uchumi eneo lake

Na Sabato Kasika

**MARA** unatajwa kuwa miongoni mwa mikoa yenye fursa nyingi za kiuchumi, kutokana na rasilimali mbalimbali zilizopo, lakini wakazi wake bado hawajanufaika na uwepo wa fursa hizo.

Miongoni mwa fursa hizo za kiuchumi ni Ziwa Victoria maliasili nyingi zikiwamo madini, vivutio vya utalii, ardhi nzuri ya kilimo na maeneo ya uvuvi, ambazo zinahitaji uwekezaji.

Hiyo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa huo, Adam Malima, ambaye sasa anawataka wakurugenzi watendaji wa halmashauri za Tarime, Serengeti, Bunda na Musoma kutenga maeneo kwa ajili ya wawekezaji.

Uwekezaji anaouzungumzia ni wa ndani, hasa kwa kujenga hoteli za kitalii za gharama nafuu, lakini zenye viwango na hadhi ya kitalii, kwamba hatua hiyo itasaidia kukuza uchumi wa maeneo.

Alitoa wito huo alipozindua kituo cha biashara cha kidijitali cha mkoa na kusema, hoteli za ndani ya hifadhi ni za gharama kubwa, hali inayosababisha watalii wa kipato cha kati na chini kushindwa kumudu gharama hizo.

"Hivyo, kujengwa hoteli zenye hadhi ya kitalii lakini zenye gharama nafuu nje ya hifadhi hiyo kutasaidia kuongezeka kwa watalii ndani ya hifadhi hiyo huku wakazi wa mkoa wakinufaika zaidi kiuchumi," anasema Malima.

Aidha, anawataka wafanyabiashara mkoani humo kuhakikisha wanautangaza mkoa wao pamoja na fursa zilizopo, ili zitambuliwe ndani na nje ya nchi, kwa manufaa ya wakazi wa Mara na taifa kwa ujumla.

Nikirejea hoja ni kwamba, hilo ndilo lengo kuu la serikali imekuwa ikihimiza kila wakati, kuhusu uwekezaji wenye lengo la kunufaisha wananchi wanaoishi kwenye eneo jirani, pia katika sura pana ya kitaifa.

Mkuu wa Mkoa, anahimiza uwekezaji katika mkoa wake. Hivyo waliopewa jukumu la kuandaa maeneo kwa ajili ya kazi hiyo, hawana budi kuzingatia hilo, kwa manufaa ya wana- mkoa kwa ujumla.

Vilevile, wafanyabiashara waliopewa jukumu la kutangaza mkoa huo na fursa zake, nao wanapaswa kuufanya kuwa sehemu yao, ili lengo la kuwainua wananchi hao mkoani kiuchumi kwa kutumia rasilimali za mkoa wao, litimie.

Ni kwa kufanya hivyo kila mahali, Tanzania itaendelea kuongoza katika uwekezaji katika ukanda wa Afrika Mashariki, kama ilivyo sasa, kwa kuvutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.18.

Hiyo inatokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali kuvutia wawekezaji, hata kukapigwa hatua kukilinganishwa na nchi nyinginezo za Afrika Mashariki.

Wakati Tanzania inaongoza, Uganda inatajwa kufuatia ikiwa na uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 700, huku Kenya ikiwa na Dola za Marekani milioni 670.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika moja ya taarifa zake za Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za ofisi yake, anasema:

"Taarifa ya Uwekezaji ya Dunia (World Investment Report) ya mwaka 2018 inayotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) imebainisha kiasi hicho kikubwa cha uwekezaji. "Taarifa nyingine ya "The Africa Investment Index (AII) 2018."

Hapo inaonyesha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 13 kati ya nchi 54 za Afrika katika kutoa fursa za masoko na vivutio vya uwekezaji.

Anasema, uhamasishaji wa miradi ya kisekta ndani na nje ya nchi, umefanikisha kuvutia uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za kimkakati na unatarajia kuwekeza mitaji ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.84 na kuzalisha ajira mpya 15,491.

Kwamba hadi kufikia Februari, 2019 miradi mipya 145 ilisajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), na 104 ambayo ni sawa na asilimia 72 inamilikiwa na wawekezaji wa ndani.

Pia, kuna miradi 38 sawa na asilimia 26 inamilikiwa na wawekezaji kutoka nje na miradi mitatu sawa na asilimia 2.01 ni ya ubia.

Hii inaonyesha ni jinsi gani uwekezaji ulivyo na umuhimu kwa maendeleo ya watu wa maeneo ambayo uwekezaji unawekwa, lakini ukilenga kunufaisha pande zote ikiwamo wananchi, mwekezaji na serikali.

BURIANI/HABARI ZA KITAIFA

# Tangulia Kibiriti, nyuma yako mbele yetu



**Na Anaeli Mbise**

ALFAJIRI ya Julai Mosi, mwaka huu, nilipokea kwa mshtuko taarifa za kifo cha Raphael Kibiriti, mmoja wa wahariri wa siasa wa Gazeti la Nipashe.

Mhariri huyo mzoefu alifariki dunia Juni 30 mwaka huu baada ya kuugua kwa muda.

Nilikutana kwa mara ya kwanza na Kibiriti mwaka 2011 katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alikokuwa anajiendeleza kitaaluma na baadaye tukafanya kazi pamoja na katika Kampuni ya The Guardian Limited hadi umauti ulipomfika.

Kibiriti, alikuwa mcheshi kazini na hata nje ya kazi. Alikuwa mwenye utu na anayejichanganya na watu wa kila rika na mwenye moyo wa kusaidia kwa hali na mali pale alipohitajika kusaidia.

Alikuwa mtu mwenye huruma 'iliyopitiliza' na katika miaka yote niliyokuwa naye UDSM na hata katika Kampuni ya The Guardian, sikuwahi kuona wala kusikia amegombana na mtu.

Tuliosoma naye UDSM tunamkumbuka kwa namna alivyokuwa na moyo wa kusaidia wenzake. Licha ya umri wake mkubwa, alichangamana na vijana na kuwasaidia kimasomo.

Kwa tuliobahatika kufanya kazi katika Gazeti la The Hill Observer linalochapishwa na SJMC, tunaendelea kukumbuka mchango wake katika kuboresha maudhui ya gazeti hilo enzi hizo.

Nitamkumbuka Kibiriti kwa kuchapa kazi. Ninakumbuka namna alivyokuwa anatekeleza majukumu yake ya kiuandishi wa habari kwa weledi, akiitumikia Kampuni ya The Guardian huku akiendelea na masomo pale SJMC.

Kibiriti alikuwa mpole, asiye na majivuno, kiongozi mzuri kwa anaowaongoza na mwepesi wa kusamehe pale alipokwazwa.

Alikuwa mtulivu katika kufanya uamuzi na mtimilifu katika uwajibikaji kwenye ngazi zote. Wakati mwingi alijipa kazi za kutoa ushauri pale tulipokuwa tumekwama kifikra, kutupatanisha tulipokuwa tumetofautiana, kututia moyo pale tulipokuwa tumekata tamaa na kutunyanyua na kutafuta uvumbuzi tulipokuwa tumeanguka.

Nitamkumbuka Kibiriti kwa mawazo yake mazuri katika uwekezaji kiuchumi, akiwa mfano mzuri wa watumishi wa umma waliowekeza pia kwenye kilimo cha pamba na mpunga Kanda ya Ziwa.

Kibiriti, aliyekuwa shabiki kindakindani wa Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam, alipenda kujifunza kutoka kwa watu wengine waliokuwa karibu naye hata kama jambo lenyewe alikuwa analijua.

Tangulia Kibiriti, nyuma yako mbele yetu!

# CHADEMA yakosa imani uchunguzi wa TAKUKURU

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema hakina imani na uchunguzi unaofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), dhidi yao kuhusu michango wanayokatwa wabunge wake.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchunguzi huo, huku wakieleza kuwa kauli za viongozi wa taasisi hiyo zinawapa shaka.

"Siku sita baada ya kupokea barua ya TAKUKURU ya Mei 21, tulipata mshangao baada ya kuwapo kwa taarifa za uongo na upotoshaji kwenye vyombo vya habari, zilizomnukuu Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbung'o akisema kuwa taasisi hiyo imewaita na kuwahoji viongozi wa CHADEMA na imepokea nyaraka kutoka kwetu," alisema.

Mnyika alidai kuwa kauli ile ya Brigedia Jenerali Mbung'o haikuwa ya kweli na kwamba walipata wakati mgumu kuelewa nia yake kwa sababu alipoitoa chama kilikuwa bado hakijawasilisha nyaraka yoyote.

"Kinyume na taratibu za kisheria, huku ikitambua kuwa haijawahi kututaarifu rasmi iwapo inatuchunguza wala haijajibu barua ya CHADEMA iliyohoji maudhui ya barua ya Takukuru ya Mei 21, mwaka huu, taasisi hiyo kupitia kwa Msemaji wake, Doreen Kapwani, ilitoa kauli nyingine.

"Kapwani alinukuliwa na vyombo vya habari kuwa taasisi hiyo imewaita kwa ajili ya kuwahoji wabunge (na waliokuwa wabunge) wa CHADEMA kwa kile alichosema ni uchunguzi ambao Takukuru Makao Makuu walikuwa wanaufanya dhidi ya CHADEMA kuhusu alichodai ni matumizi mabaya ya fedha za michango ya wabunge."

Mnyika alitaja nyingine ni ya Juni 17, wakati Bunge likivunjwa ambapo alidai Brigedia Jenerali Mbung'o alitoa kauli ya kushabikia chama cha siasa na alikwenda mbali na kuwahamasisha wapiga kura kuwa wanapopiga kura mwaka huu basi wakumbuke miradi mikubwa ambayo imefanywa na Serikali.

Alisema kitendo hicho kimewaongezea shaka kuwa sasa taasisi hiyo nayo imeingia kwenye kutekeleza kauli iliyotolewa na Katibu Mkuu wa CCM kuwa watatumia vyombo vya dola kuendelea kubakia madarakani.

Mnyika aliendelea kueleza kuwa hata hicho TAKUKURU wanachokiita ni uchunguzi wanaona ni kauli zilizotolewa kisiasa, kwa malengo ya kisiasa na waliokuwa wabunge wa Chadema, ambao baada ya kufukuzwa au kujiondoa wenyewe na kujiunga na mahasimu wao wa kisiasa.

"Kuanzia hapo TAKUKURU ikazidandia na kuita kuwa ni malalamiko," alisema.

Aidha, alisema licha ya Juni 27, TAKUKURU kutangaza kuwa wamekamilisha uchunguzi lakini wameletewa barua tatu mfululizo na miongoni mwa vitu wanavyovitaka ni pamoja na nyaraka mbalimbali za chama za kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2020.

Mei 21, Takukuru iliitaka CHADEMA ifikapo Mei 28, iwasilishe nyaraka na taarifa za hesabu za serikali zilizokaguliwa za miaka ya fedha 2015/16, 2016/17, 2017/18 na 2018/219.

"Walitutaka tuwasilishe mwongozo na kanuni za chama inayotoa idhini ya kuwakata wabunge fedha hizo kwa mwezi, nyaraka za stakabadhi cha chama kukiri kupokea makato ya fedha za wabunge na muhtasari ya chama inayoonyesha makubaliano ya chama ya kuwakata wabunge hao," alisema Mnyika na kuongeza:

"Tuwasilishe Katiba na kanuni za chama zilizotumika kati ya mwaka 2015 hadi sasa, muhtasari ya chama zinazoonyesha kutumika kwa fedha hizo walizokatwa na nyaraka za mapato na matumizi ya fedha hizo."

Alisema kulingana na muhtadha wa barua hiyo, Mei 26, CHADEMA ilijibu TAKUKURU kuwa hakuna mahali popote inaeleza taasisi hiyo inachunguza kosa au makosa au nyaraka wanazohitaji ni kwa ajili ya kusaidia uchunguzi wa kosa gani.

"Tuliwaandikia TAKUKURU kuwa ikiwa kuna kosa au makosa au kesi ambayo ofisi hiyo inafanya uchunguzi wanaweza kuwasilisha hati nyingine inayokidhi vigezo na matakwa ya kisheria ndipo chadema itawasilisha kulingana na matakwa ya uhitaji.

"Pamoja na kuweka zuio hilo CHADEMA ilitoa ushirikiano wote uliohitajika ikiwamo kuwasilisha nyaraka zote hitajika pamoja na kwamba ziliombwa kinyume cha utaratibu."

Mnyika alisema baada ya kupokea barua hiyo ya Takukuru, chama kiliamua kukaa kimya kikiamini kuwa uchunguzi unaofanyika utakuwa wa kitaalam na huru lakini wameanza kuona viashiria vya malengo 'fulani' ya kisiasa hasa kwa muktadha wa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, mwaka huu.

Alisema mpaka sasa ni zaidi ya mwezi mmoja na katika kipindi chote walikuwa na mawasiliano ya kikazi kuhusu kile walichokiita uchunguzi.

"Hadi tunapozungumza, taasisi hiyo imehoji zaidi ya watu 60 wakiwamo wanachama wa CCM katika suala walilotuandikia wakitaka ushirikiano wetu," alisema.

**KAULI YA TAKUKURU**

Nipashe ilipomtafuta Kapwani kuzungumzia malalamiko hayo ya TAKUKURU, alisema hawawezi kujibu mpaka watakapoona taarifa iliyotolewa na CHADEMA.

# Naibu Waziri apongeza wafanyakazi wa CCBRT

**Na Mary Mshami, UDOM**

SERIKALI imewapongeza wafanyakazi wa Hospitali ya CCBRT iliyoko Msasani, jijini Dar es Salaam, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhudumia jamii.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Godwin Mollel.

Naibu Waziri huyo lifanya ziara ya kushtukiza katika hospitali hiyo na kueleza kuridhishwa na utendaji wao.

"Nawapongeza kwa kazi nzuri, kama serikali tunatambua mchango wenu," alisema Naibu Waziri huyo na kuendelea:

"Leo nimefika kusalimia kidogo, nitakuja wakati mwingine tujadili kwa kina."

Naye Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi, alimshukuru Naibu Waziri Mollel kwa kuitembelea taasisi yao pamoja na ushirikiano wanaopata kutoka Wizara ya Afya.



Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano wa Benki ya NMB, Eunice Chiume, akizungumza na waandishi wa habari katika Banda la NMB lililopo kwenye Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. Benki hiyo, imewasogezea huduma zote za kifedha wananchi wote wanaohudhuria maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aonya fidia ndogo ardhi

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuacha tabia ya kupora maeneo ya wananchi pasipo fidia au kutoa fidia kidogo kwa kisingizio cha ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Lukuvi alitoa rai hiyo jana akiwa mkoani Kigoma wakati wa uzinduzi wa ofisi za ardhi za mkoa huo, akiwataka wakurugenzi pindi wanapopanga mipango ya maendeleo, wahakikishe wanajumuisha na fedha za kulipa wananchi fidia ili kuondoa migogoro mingi ya ardhi.

"Marufuku kwa wakurugenzi wa halmashauri au kiongozi yeyote wa taasisi za umma kuchukua maeneo ya wananchi, mkipanga mipango ya maendeleo ya kujenga hospitali au shule, hakikisheni mna fedha za fidia," aliagiza.

Lukuvi alikemea tabia ya halmashauri kutoa fidia kidogo kwa wananchi pindi wanaponunua maeneo yao kisha kuyauza kwa bei kubwa inayowanufaisha wao zaidi tofauti na uhalisia wa fidia waliyopewa, akitolea mfano fidia ya Sh. 1,000 kwa kila mita za mraba kisha wahusika kuuza tena kwa Sh. 10,000 kwa mita za mraba.

Akizungumzia makusanyo ya kodi ya ardhi kwa Mkoa wa Kigoma, Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoani humo, Chediel Mrutu, alisema bado hayaridhishi kwa kuwa kwa sasa wako asilimia 59.66. Alisema moja ya vikwazo vilivyoko katika ukusanyaji mapato ni uhaba wa watumishi na uwapo wa taasisi za umma zinazomiliki maeneo makubwa, lakini hazilipi kodi.

Chediel aliiomba wizara kuona namna ya kusaidia jambo hilo ili mapato ya kodi ya ardhi katika maeneo yanayomilikiwa na taasisi za serikali, ili kuzuia ucheleweshwaji au kutokulipa kodi.


**TUKUYU SPRINGS WATER LTD**

**JOB OPPORTUNITY**

**TUKUYU SPRINGS WATER COMPANY LTD**, a newly established bottling Company located about five kilometers from Tukuyu Town, Rungwe District is seeking to recruit **Sales and Marketing Officers.**

Suitable candidates for the positions are requested to submit their detailed resumes (CVs) and relevant certificates to the email address provide below.

The shortlisted candidates will be invited for interviews during which they will be able to provide more information on their experiences and professionalism.

Successful candidates will be responsible for meeting the sales and marketing targets of the bottled water products. They will also be responsible for promoting the products through events, visits, exhibitions, advertising so as to increase the visibility of the Company and its products and make them known to the public, targeted clients or potential customers

**Qualifications:**
- Holder of at least a first degree in Marketing or Business Administration with a strong marketing bias
- At least 2 years' experience in sales and marketing, one of which should preferably be in beverage or food industry

Send to Email address: tukuyuspring@yahoo.com.
Deadline: 15 July, 2020


## Wizara yabainisha vikwazo uwekezaji mbolea

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amesema changamoto zinazowakabidili wawekezaji wa mbolea nchini, zinaweza kupatiwa ufumbuzi kwa kuimarisha Sheria ya Mbolea namba 9 ya mwaka 2009 inayohusu uwekezaji na usimamizi wa mbolea nchini.

Alisema sheria hiyo itaboreshwa kwa kuundwa jopo la wizara ili kuimarisha uhusiano na Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Kusaya aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kikao cha wadau wa chai kwa ajili ya kujadili mbolea ya Minjingu chai zinazozalishwa nchini.

Alisema mpango huo utasaidia kutatua changamoto kubwa zinazowatesa wawekezaji wa mbolea ambazo ni gharama za uwekezaji zinazofanya mbolea zinazozalishwa nchini kuwa na bei kubwa kuliko zinazoingia nchini.

Kusaya alisema pia kuwapo na mifumo ya kisheria yenye utata ambayo inamlazimisha mwekezaji kushughulikia masuala mengine yanayoweza kufanywa na taasisi nyingine.

Kusaya alisema kwa sasa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), ina jukumu la kuboresha mazingira ya uwekezaji katika viwanda na kuboresha sheria ya mbolea na miongozo inayohamasisha wawekezaji waliopo kuzalisha kulingana na uwezo wa kiwanda.

Alieleza kuwa, TFRA inaendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba viwanda vyote vya mbolea na visaidizi vyake vinasajiliwa na kuwa na leseni hai muda wote.

Katibu Mkuu huyo alisema pia TFRA inashirikiana na Taasisi za utafiti na wadau wengine wa maendeleo katika kuelimisha umma juu ya umuhimu wa matumizi sahihi ya mbolea.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephen Ngailo, alisema jumla ya upatikanaji wa mbolea nchini ni tani 544,162 sawa na asilimia 93 kwa mwaka 2019/20 wakati mahitaji ya nchi yalikuwa ni tani 586,604.

## 2,880 zathibitisha kushiriki Sabasaba

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI 2,880 zimethibitisha kushiriki Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ambayo yalianza Julai Mosi katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho hayo.

Alisema kwenye maonyesho hayo yanayotarajiwa kufunguliwa rasmi leo na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kampuni 2,835 ni za Watanzania na 43 ni kutoka nje.

"Kama Watanzania mnavyofahamu tulikuwa na ugonjwa wa corona na baadhi ya nchi zilijifungia, lakini hata hivyo Tanzania tumefanikiwa kumtanguliza Mungu na tumeshinda na watu wamejitokeza kwa wingi kwenye maonyesho haya," alisema Waziri.

Bashungwa alisema Rais John Magufuli aliwaongoza vyema Watanzania kwenye kupambana na ugonjwa huo na ndiyo sababu hata ushiriki wa washiriki kwenye maonyesho hayo umeendelea kuwa mkubwa.

Alisema ingawa baadhi ya washiriki kutoka nje wameshindwa kuja wametumia teknolojia ya elektroniki kwa washiriki hao kushiriki mikutano itakayofanyika kwenye maonyesho hayo bila kulazimika kuja nchini.

Alisema Tanzania imekuwa nchi ya kipato cha kati kabla ya mwaka 2025 uliotarajiwa kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Magufuli katika utekelezaji wa Ilani ya CCM waliyoinadi kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Alisema Watanzania wanapaswa kujipanga kwenda kwenye ujenzi wa viwanda na uchumi endelevu kwani licha ya janga la corona msingi uliowekwa wa ujenzi wa viwanda umesababisha uchumi kutotikisika.

Alisema baada ya kuingia kwenye uchumi wa kati Watanzania wanapaswa kuchapa kazi na kuzalisha bidhaa i zenye ubora wa hali ya juu.

# Wachina wasota rumande kesi ya uhujumu uchumi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

RAIA wanne wa China wameendelea kusota rumande kutokana na upande wa Jamhuri kutokamilisha upelelezi wa makosa matatu ya uhujumu uchumi yanayowakabili.

Akisoma shauri hilo namba 38 la mwaka 2020 mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Morogoro, Ester Ushacky, Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, alisema upelelezi wa shauri hilo unaendelea, hivyo alimwomba hakimu lipangiwe siku nyingine hadi upelelezi utakapokamilika.

Kutokana na kutokamilika kwa upelelezi Hakimu Ushacky, alikubali ombi hilo na kuamua kuwa litasomwa tena Julai 13, mwaka huu.

Juni 16 mwaka huu washtakiwa hao, Wang Zhen, Li-yu, Chen Maoan na Bangshum Zhing, walifikishwa kwenye mahakama hiyo, ambapo wakili mafuru aliieleza mahakama kuwa wanakabiliwa na makosa matatu.

Alidai kosa la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia fedha kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi sura ya 200 marekebisho ya mwaka 2002.

Shtaka la pili ni kuhifadhi fedha kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi sura ya 200 marekebisho ya mwaka 2002.

Mafuru alitaja shtaka la tatu ni kuondoa sarafu kwenye mzunguko wa fedha kinyume cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 marekebisho ya mwaka 2019.

Ilidaiwa kuwa watuhumiwa walitenda makosa hayo kwa pamoja Mei 9 mwaka huu eneo la Mwere Manispaa ya Morogoro.



Meneja wa Kiwanda cha Tanzania Breweries Malting Plant cha Mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, Joseph Mwaikasu (kulia), akitoa maelezo ya uendeshaji wa shughuli za kiwanda kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), alipokitembelea, jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mauzo wa TBL, Kanda ya Kaskazini na Ziwa, James Bokella. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanyasu atoa neno hoteli kufunguliwa

**Na Hemed Lusungu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amepongeza uamuzi wa Hoteli ya Serena kufunguliwa tangu ilipofungwa kwa ajili ya kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona. Alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam wakati akishiriki hafla ya kufungua hoteli ya Serena ambayo imekuwa ni muhimu katika kuwahudumia watalii wengi wanaotoka na kuingia kutoka nchi za nje kabla na baada ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Alisema uamuzi wa kufungua hoteli hiyo unatoa ujumbe mzito duniani kuwa Tanzania ipo salama na ipo tayari kwa ajili ya kuwapokea watalii.

Alisema kurudi kwa biashara hiyo kunarudisha uhakika wa maisha ya watu takribani 450,000 ambao wameajiriwa moja kwa moja katika sekta ya utalii.Alisema ugonjwa wa corona uliiathiri jamii katika nyanja za kiuchumi na kijamii baada ya watu wengi kupoteza ajira na wengine kuachishwa kazi.

Alisema uamuzi wa kuifungua Hoteli ya Serena unaleta mwanga wa matumaini kwa Watanzania wanaoitegemea sekta ya utalii katika kuendesha maisha yao.

"Ninawashukuru Hoteli ya Serena kwa kupeleka ujumbe kwa wawekezaji wetu wote ambao wanaogopa na kufunga biashara zao kwa ajili ya ugonjwa huo.

Kanyasu alitoa wito kwa jamii kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona na kuwa ugonjwa huo bado upo, lakini hauwezi kukimbiwa, hivyo ni lazima kujifunza kuishi nao.

"Tunamshukuru sana Rais John Magufuli kwa kufanya maamuzi ya kufungua anga, ambapo tunaamini biashara ya utalii na biashara ya anga zinategemeana kwa kiasi kikubwa," alisema.

Alisema uamuzi huo umeifanya biashara ya utalii kurejea kwa kuwa tayari ndege za mashirika ya ndege ya Ethiopia, Emirates, KLM na Quatar zimeanza kuja nchini.

Naye, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Goldwin Mollel, aliwataka wadau wa sekta ya utalii kuchukua tahadhari kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa na wizara yake ili kuhakikisha usalama wa wageni na wenyeji wanaowahudumia watalii.

Akizungumzia uamuzi wa kuifungua hoteli hiyo, alisema inatuma ujumbe kwa wawekezaji wengine kuwa Tanzania ipo salama na Watanzania wapo tayari kwenda nchi za nje kwa ajili ya kutafuta shughuli za biashara.

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania, Jaji mstaafu, Thomas Mihayo, alisema tangu anga lilipofunguliwa kumeonyesha dalili njema ya ujio wa idadi kubwa ya watalii.

"Kuna matumaini makubwa ya kupata watalii wengi zaidi kwa mfano siku ya jana ndege ya Shirika la KLM ilitua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro ( KIA) ikiwa na abiria 200 kati ya hao 45 ni watalii waliokuja nchini kwa ajili ya kutalii," alisema Jaji mstaafu Mihayo.

## Segerea walalamikia mrundikano wa taka

**Na Faudhia Sultan,** UDOM

WAKAZI wa Mtaa wa Mangumi, Tabata Segerea jijini Dar es Salaam, wamelalamikia uongozi wa serikali za mitaa juu ya ucheleweshaji wa gari la takataka na kusababisha uchafu na harufu katika baadhi ya maeneo.

Akizungumza na wananchi juzi, Mwenyekiti wa Mtaa huo, Mohamedi Kawambwa, alisema alipokea malalamiko ya uchafu na harufu inayowakumba baadhi ya wakazi wa eneo hilo.

"Malalamiko mengi yametufikia katika ofisi yetu na tupo katika taratibu za kufuatilia suala hili. Gari la takataka uchelewaji wake unatokana na nguvu yetu wananchi wenyewe katika ulipaji, hivyo endapo gari halikuja mwezi mzima ni sisi wenyewe na sio gari hilo," alisema Kawambwa.

Aliongeza: "Nawaomba wakazi wa Mangumi kuwa na ushirikikiano wa kutoa pesa kwa wakati ili gari la takataka liweze kuja na kusafisha mazingira yetu kwa muda mwafaka."

Mmoja wa wakazi wa mtaa huo, Mwanahamisi Mussa, alieleza jinsi harufu ya takataka hizo ilivyodumu muda mrefu, hivyo kuwakera na kuhatarisha maisha hasa kwa watoto. Kadhalika Mwenyekiti wa mtaa huo alisema ataweka utaratibu juu ya ukusanyaji wa takataka hizo ndani ya siku mbili ili kuepusha uchafuzi na urundikaji wa takataka katika mtaa huo.

## Vyuo vyahimizwa diplomasia ya uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa (CFR) kimependekeza vyuo vishirikiane ili Tanzania inufaike na diplomasia ya uchumi ambayo ndiyo chagizo la dunia katika kipindi hiki. Akizungumza kwenye hafla iliyojadili mwelekeo wa dunia kiuchumi jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa chuo hicho, Dk. Jeremia Ponera, alisema chuo chao kinatoa mafunzo ya ngazi mbalimbali katika masuala ya uchumi, biashara na uhusiano wa kimataifa, na amewataka Watanzania kutumia fursa ya kuwapo mafunzo hayo.

"Wakati huu ambao dunia nzima inazungumzia diplomasia ya uchumi, itakuwa haina maana sana ikiwa Watanzania hatutaitafsiri dhana hiyo kwa vitendo. Nawaomba Watanzania wajiunge na kozi fupi na za muda mrefu ili kujitengenezea uwezo kiushindani na mataifa mengine, alisema Dk. Ponera.

# Atiwa mbaroni kwa madai ya kushawishi na kupokea rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, imemburuza mahakamani Joseph Mwenda kwa tuhuma za kushawishi na kupokea rushwa zaidi ya shilingi milioni 15.

Kosa hilo ni kinyume cha kifungu cha Sheria ya Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alibainisha hayo jana mjini Kibaha alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari.

Suzana alisema, mtuhumiwa huyo alipokea fedha hizo kutoka kwa mwananchi kwa madai kuwa ziliombwa na ofisa wa TAKUKURU ili aweze kumsaidia mtuhumiwa huyo kwenye kesi yake.

Mkuu wa TAKUKURU alisema, taasisi hiyo ilipata taarifa kutoka kwa msamaria mwema kuhusiana na anachokifanya Mwenda ndipo walipojipanga na kufanikiwa kumkamata.

Suzana alisema, uchunguzi dhidi ya mtuhumiwa huyo unaendelea ili kubaini malengo yake na watu ambao tayari amewatapeli.

Alitumia nafasi hiyo kuwaasa wananchi kutoa taarifa mara wanapopigiwa simu na mtu yeyote atakayejitambulisha kuwa ni ofisa wa TAKUKURU na kudai fedha au kutaka kuonana eneo ambalo sio ofisi ya taasisi hiyo.

# Lukuvi awashukia viongozi uporaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** KATAVI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amekerwa na tabia ya baadhi ya viongozi kuhusika kupora ardhi ya wananchi, akionya kuwa dawa yao iko jikoni.

Amesema tabia hiyo iko mbioni kukomeshwa kutokana na watendaji wa sekta ya ardhi kuhamishiwa wizarani sambamba na kuanzishwa ofisi za ardhi katika mikoa. Waziri Lukuvi alisema hayo juzi wakati wa kuzindua ofisi ya ardhi Mkoa wa Katavi wilayani Mpanda, ikiwa ni mfululizo wa uzinduzi wa ofisi za ardhi kwenye mikoa mbalimbali nchini. Alisema wapo baadhi ya viongozi wa wilaya na mkoa ambao ni sehemu ya migogoro ya ardhi na wamekuwa wakitumia madaraka yao vibaya kwa kupora na kuuza ardhi ya wananchi.

Lukuvi aliweka wazi kuwa tabia hiyo inamkera Rais John Magufuli na katika kushughulikia tatizo hilo, wameona kuna haja ya kuchukua hatua kwa kuanzisha ofisi kila mkoa.

Kwa mujibu wa Lukuvi, uanzishwaji ofisi za ardhi za mikoa pamoja na uhamishaji watendaji wa sekta ya ardhi kutoka Tamisemi kwenda Wizara ya Ardhi, kunatoa nguvu kwa watumishi wa sekta ya ardhi kutumia na kusimamia sheria.

"Kuna viongozi wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa wanaotumia madaraka yao vibaya kwa kupora ardhi ya wananchi. Safari hii hakuna fursa hiyo maana watendaji wote wa sekta ya ardhi wako chini ya Wizara ya Ardhi, madiwani hawawezi tena kuazimia kuwafukuza," alisema. Akizungumzia upimaji ardhi katika Mkoa wa Katavi, Lukuvi aliagiza hadi kufikia mwisho wa mwaka huu, vijiji vyote katika mkoa huo viwe vimepimwa na kupatiwa hati za kijiji sambamba na wamiliki 15,000 waliokwama kupewa hati kutokana na urasimu, kupatiwa hati zao.

Alisema kuwa kwa sasa, hakuna visingizio vya kuchelewa kutoa hati hizo kwa kuwa vifaa kwa ajili ya upimaji vipo.

Lukuvi aliuagiza mkoa huo kupima ardhi na kutoa hati baada ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Katavi, Siyabumi Mwaipopo, kusema kuwa kati ya vijiji 172 vilivyoko kwenye mkoa huo, vijiji vitatu tu vilivyopimwa na kupatiwa hati za vijiji.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mshauri Mkuu wa Mpango mpya wa kukuza utalii wa ndani, Dk. Fenella Mukangara, wakati wa uzinduzi wa mpango huo jijini Dar es Salaam katikati ya wiki. Anayeshuhudia ni mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT), Dk. Costantino Bushungwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kigwangalla azindua mpango mpya kukuza utalii wa ndani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, amezindua mpango mpya wa kukuza utalii wa ndani unaojulikana kama Domestic Tourism Promotion Initiative (DTPI), huku akitoa wito kwa Watanzania hususani vijana kushiriki zaidi kwenye sekta hiyo.

Mkakati huo wenye kaulimbiu 'Utalii Mpya, Fursa Mpya' unaratibiwa kwa pamoja baina ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT), kampuni ya Real PR Solutions ya jijini Dar es Salaam, BRAJEC, pamoja na kampuni ya Peak Performance.

Uzinduzi huo uliofanyika jijini Dar es Salaam ulihusisha na viongozi wengine waandamizi kutoka serikalini na pamoja na wadau wa utalii nchini wakiwamo Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Chama cha watoa huduma za utalii wa ndani (TLTO) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Wengine ni Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA), Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), viongozi waandamizi kutoka Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na Shirika la Ndege la Precision Air pamoja na wadau wengine.

Dk. Kigwangalla alisema mpango huo umekuja wakati mwafaka wakati ambapo serikali imejizatiti kuhakikisha sekta hiyo inamilikiwa kwa kiasi kikubwa na wadau kutoka ndani ya nchi wakiwamo wawekezaji wadogo ili kutoa fursa za ajira na kutoa nafasi kwa wadau hao kushiriki kukuza sekta hiyo.

"Katika kufanikisha ushiriki wa wawekezaji wazawa hususani wale wadogo wadogo kwenye sekta ya utalii, serikali iliamua kushusha tozo mbalimbali na masharti ambayo yalikuwa kikwazo kwa wadau hao kushiriki kwenye sekta hii muhimu."

Alisema uamuzi huo wa serikali umewezesha ongezeko kubwa la wadau hao kushiriki kwenye sekta ya utalii, kwa wa mwaka 2019 idadi ya wawekezaji kwenye sekta hiyo iliongezeka kutoka 1,100 hadi takribani 2,000 ambapo 600 kati ya hao ni wawekezaji wapya wazawa.

Mshauri Mkuu wa Mpango huo, Dk. Fenella Mukangara, alisema mpango huo unaohusisha juhudi mahsusi katika kusaidiana na serikali kukuza utalii wa ndani na kupunguza athari za janga la corona kwenye sekta hiyo muhimu.

Alitaja baadhi ya mambo muhimu kwenye kampeni hiyo ambayo yatatekelezwa kwa awamu kuwa ni mafunzo kwa vijana kote nchini ili waweze kunufaika na mnyororo wa thamani katika sekta ya utalii ikiwamo kuongoza watalii, mafunzo ya huduma kwa wateja katika hoteli na migahawa, vyombo vya usafiri na ujuzi wa kufungua kampuni za utalii.


"Tunatarajia mafunzo haya yatawanufaisha vijana zaidi ya 100,000 hususani wale wasio na ajira ili waweze kutambua fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii na wazitumie vizuri."

Aidha, Dk. Mukangara alitaja mikoa itakayoanza kunufaika na mpango huo ni Kanda ya Ziwa ikiwamo Mwanza, Geita, Kagera, Simiyu, Mara na Shinyanga.

Alisema katika kuupamba mkakati huo kutakuwa na uhusishwaji wa matukio mbalimbali ya michezo na burudani ili kuvutia walengwa zaidi wa mpango huo. Matukio hayo ni pamoja na mbio za Capital Mountain Run zitakazofanyika katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Pia mdahalo wa masuala ya utalii na uwekezaji Kanda ya Ziwa (Lake Zone Tourism and Investment Symposium) utakaofanyika jijini Mwanza.

Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT) Dk. Costantino Bushungwa, alisema chuo kimejipanga kuhakikisha kinawaandaa kitaalamu wadau wa utalii ili waweze kutambua fursa zitokanazo na sekta hiyo muhimu na waweze pia kunufaika.




Ukurasa 13

Utamaduni wa Mtanzania leo hii uko wapi?

BUFE
IJUMAA JULAI 3, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

## Wataalamu: Watumishi viwanda nyama wako jirani sana na corona

# Tanzania ya JPM ilivyofanikiwa kuiona hatua Uchumi wa Kati

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI Tanzania ilitangazwa rasmi kuwa katika Uchumi wa Kati. Ni miezi mitano kabla ya kumaliza awamu yake ya kwanza ya uongozi, Rais Dk. John Magufuli (pichani) na siku moja baada ya kurejesha fomu ya chama chake kuomba apitishwe kuwania tena, azma aliyotangaza kuinuia, imetimia.

Hiyo ni kupigania Tanzania kuingia katika orodha ya uchumi wa kati, mwenyewe akitabasamu kupokea hadhi hiyo kutoka ya Benki ya Dunia, kwamba ni ushindi wa Watanzania wote.

Utaratibu wa Benki ya Dunia, hutangaza mabadiliko ya hadhi hiyo kila Julai Mosi wa Mwaka na tovuti yake inataja nchi zingine zilizopanda ya hadhi kutoka kundi la nchi masikini na kuingia uchumi wa kati ni Nepal na Benin.

Kimsingi, Benki ya Dunia hutambua hadhi ya nchi kiuchumi kwa kuzigawa katika makundi: Ngazi ya juu; ngazi ya kati iliyoko katika kundi la chini na juu; na nchi zenye uchumi wa chini, maarufu kama nchi masikini.

Namna inavyopatikana kiwango cha uchumi wa nchi, ni kupitia hisabati ya kugawanya pato la taifa kwa idadi ya wananchi wa waliopo na kupata wastani wa pato la mtu mmoja mmoja kitaifa.

Wastani uliotengwa kwa mataifa ya uchumi wa kati kwa kiwango cha chini ambako Tanzania imo, ni yenye wastani wa pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja, kati ya Dola za Marekani 1006 (Sh. 2,330,902) na 3,955 (Sh. 9,163,735).

Pia, pato la taifa la kati katika ngazi ya juu, ni kwa kwenye wastani za Dola za Marekani 3,956 (Sh. 9,166,052) na 12,235(Sh. 28,248,495); na nchi zenye chini ya Dola za Marekani 1006, inaangukia katika kundi la nchi za uchumi wa chini.

Benki ya Dunia imeitaja Tanzania kufika hatua hiyo ya mafanikio, baada ya kuwa na pato la taifa la wastani wa mtu mmoja Dola za Marekani 1080, sawa na Sh. 2,502,543.60



### JEDWALI LA BENKI YA DUNIA

| Uchunmi | Kundi jipya | Kundi la zamani | Pato kwa mtu (Dola za Marekani) Julai 1, 2020 | Pato kwa mtu (Dola za Marekani) Julai Julai 1, 2019 |
|---|---|---|---|---|
| Benin | Uchumi Kati (chini) | Uchumi chini | 1,250 | 870 |
| Indonesia | Uchumi Kati (juu) | Uchumi Kati (chini) | 4,050 | 3,840 |
| Mauritius | Uchumi wa Juu | Uchumi Kati (juu) | 12,740 | 12,050 |
| Nauru | Uchumi wa Juu | Uchumi Kati (juu) | 14,230 | 11,240 |
| Nepal | Uchumi Kati (chini) | Uchumi chini | 1,090 | 960 |
| Romania | Uchumi wa Juu | Uchumi Kati (juu) | 12,630 | 11,290 |
| Tanzania | Uchumi Kati (chini) | Uchumi chini | 1,080 | 1,020 |

**VIGEZO VINGINE**

Katika maelezo yake, Benki ya Dunia, imeorodhesha vigezo vingine vinavyotiwa maanani kama vile mfumuko wa bei, kiwango cha mabadilishano ya fedha za kigeni, pato la taifa na kasi ya ukuaji uchumi, kukiwepo mapitio ya kina kuhusu nyendo za nchi.

"Mapitio ya ki-nchi yamesaidia sana katika kufanya mapitio kwa mataifa ya Benin, Nauru na Tanzania," inaeleza taarifa hiyo.

**MCHAMBUZI**

Mchambuzi wa masuala ya kiuchumi, Deus Kibamba aliyehojiwa na shirika la habari la BBC, anafafanua benki hiyo hutathmini pato la taifa, mathalan jumla ya utajiri wa rasilimali na ule wa kifedha na kugawanya na idadi ya watu wa nchi.

Kibamba anasema hiyo ina tafsiri kwamba, taifa husika linaelekea kuimarika kiuchumi na ishara kwamba siasa za nchi zinaenda sambamba na ukuaji kasi ya ukuaji uchumi, sifa inayosaidia kuvutia uwekezaji mitajio ya kigeni nchini, hali inayochangia kuimarika uchumi.

Hata hivyo, Kibamba anakumbusha mafanikio hayo yana maana kwa kwamba, Watanzania kwamba, ili wanufaike na hatua hiyo wanahitaji kuingeza juhudi za kuifanya kazi kwa mtu mmoja mmoja, ili kuboresha uchumi zaidi.

Benki ya Dunia inafafanua kuwa mataifa yenye kipato cha kati ndio yenye asilimia 75 ya idadi ya watu duniani, hali kadhalika asilimia 62.

BIASHARA

# Wataalamu: Watumishi v nyama wako jirani sana

- Sauti kubwa, kuongea, kelele, mate...zimo

Na Mwandishi Wetu

MARADHI corona ambayo si jambo geni kwa umma na kimataifa sasa, kijamii inaguswa kwa kiwango kikubwa na namna yake kati ya sehemu moja na nyingine.

Inapozungumziwa kada ya watumishi katika sehemu mbalimbali za kazi, kuna nafasi ya pekee viwandani, ambako kimataifa nako hawajaachwa salama.

Hadi sasa kuna mamia ya wafanyakazi wamepatikana na virusi vya corona katika kampuni za kutengeneza nyama na maeneo ya machinjioni hasa katika nchi za Ulaya na Bara Marekani, kwa uchache kutaja Ujerumani, Ufaransa, Hispania na Uingereza.

Ni maeneo ambako kuna milipuko mikubwa, kunatolewa takwimu za jumla ya wafanyakazi 150 wameshaambukizwa virusi vya corona.



Kazi zikiendelea ndani ya viwanda tofauti vya kuandaa nyama, mazingira yanayolalamikiwa na wataalamu kuwa na uhusiano wa karibu na corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**VIWANDA NYAMA**

Bev Clarkson, kutoka Chama cha Wafanyakazi nchini Uingereza, ana ufafanuzi wake akitamka:"Chama hiki kimekuwa kikitahadharisha kila wakati kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kutokea mlipuko wa virusi vya corona Uingereza, hasa katika kampuni za kutengeneza nyama".

Pengine katika msingi wa hoja hiyo, inaweza kuibua swali lake, ni kwa nini wafanyakazi wa kampuni za nyama ndiyo wanapata virusi vya corona?

Majibu yanayotolewa ni kwamba wahusika katika eneo hilo wanapata virusi kutokana na matone ya mate yanayoruka mdomoni, yanayoweza kusababisha kukohoa, kucheua au hata aliyeambukizwa akasambaza virusi hivyo kirahisi.

Inabashiriwa kwamba, maambukizi hayo huenda yakatokea baada ya kukaribiana na aliyeambukizwa au kugusa sehemu iliyopata maambukizi. Profesa Lawrence Young, kutoka Chuo Kikuu cha Warwick anafafanua zaidi:

"Viwandani, maeneo ya ndani ambayo huwa ni baridi sana na yenye unyevunyevu, yana mazingira yanayopendwa na virusi vya corona na kuchangia virusi hivyo kukaa kwa muda mrefu na kusambaa."

Anaendelea kwa kutahadharisha kwamba: "Virusi vinavyosambazwa kwa matone yanayoruka kutoka kwa watu walioambukizwa, huenda vikaendelea kusambaa kwa muda mrefu."

Lingine lialochukuliwa kama angalizo katika maeneo ya kazi yenye majokofu, ni kwamba mashine zinazonguruma kwa sauti ya juu, huendana na kuwafanya wafanyakazi nao walazimike kuzungumza kwa sauti ya juu.

> **“ Viwandani, maeneo ya ndani ambayo huwa ni baridi sana na yenye unyevunyevu, yana mazingira yanayopendwa na virusi vya corona na kuchangia virusi hivyo kukaa kwa muda mrefu na kusambaa**

Profesa Young, anaongeza kuwa hiyo ina mchango mkubwa katika kuongeza usambazaji matone ya mate kirahisi kutoka kwa waliopatwa na maambukizi.

**MAZINGIRA YA KAZI**

Kuna msisitizo mwingine kuwa ni muhimu sana, wafanyakazi wakawa katika umbali wa mita mbili kati ya mmoja na mwingine, wakati wanapofanya kazi zao katika viwanda vyenye shughuli nyingi.

Pia , kunatajwa kuwa suala la jumla la ukosefu wa jua kunaweza kusaidia virusi kuendelea kuwa hai kwa muda mrefu zaidi.

"Wakati watu wanakaribiana wakiwa wanafanya kazi, sababu bila shaka hii ni kazi ngumu huku wakiwa wanahema kwa nguvu, kuna uwezekano mkubwa wa kusambaa virusi kutoka kwa mtu mmoja aliyeambukizwa hadi kwa wengi walio karibu nae," amesema Tara Smith, Profesa wa masuala ya kuambukizwa chuo kikuu cha Kent, Ohio.

Hata hivyo hakuna ushahidi unaoonesha kwamba bidhaa za nyama zinaweza kuwa chanzo cha maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa covid-19 viwandani.

Shirika la Kudumisha Viwango vya Chakula, linaunga mkono kuwepo uwezekano mdogo wa kupata virusi vya corona kutoka kwenye vyakula, kwa sababu ugonjwa huo hausambazwi kwa njia hiyo.



# viwanda
# na corona

**KIWANDA NYAMA**

Sio tu hali ilivyo ndani ya viwanda ndiyo vinaweza kuongeza hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya corona, Michael Head, Mtafiti Mwandamizi wa Afya katika Chuo Kikuu cha Uingereza Southampton, Uiongereza, anafafanua:

"Baadhi ya viwanda hivi vina makazi karibu na wakati mwingine chumba kimoja ni makazi kwa wafanyakazi kadhaa. Pia, inawezekana wafanyakazi wanasafirishwa kwa basi hadi maeneo ya kufanya kazi na watakuwa pamoja kwa siku nzima."

Chama cha Wafanyakazi kinasema, ingawa kinawakilisha wengi katika kampuni ya kutengeneza nyama, mara nyingi wafanyakazi wa viwanda hivyo ni raia wa kigeni ambao huenda wawana likizo na mtu anapokuwa mgonjwa, kuna uwezekano akakosa pesa zinazomuwezesha kujikimu wakati anajitenga nyumbani baada ya kuugua.

Chama hicho kinasema watu hao mara nyingi huwa hawazungumzi Kiingereza kama lugha yao rasmi na wana wasiwasi kupoteza ajira zao, jambo linalowafanya kunyamaza hata wanapokuwa wagonjwa.

**MWONGOZO SERIKALINI**

Serikali imetoa mwongozo wa kuwa na mazingira salama ya kufanya kazi katika kampuni za kutengeneza vyakula, ikiwamo kutokaribiana kwa angalau umbali wa mita mbili.

Pia, kuna miongozo viwanda wa kufanyika usafi wa kila mara, kutenga wafanyakazi wanaoonyesha dalili na kuwapo muda wa kuanza, pia kupumzika.

Lingine lionatajwa kuwa ni mapendekezo ya mavazi yanayomkinga mtu na virusi uwezekano wa kupata virusi, huku wafanyakazi wa kampuni ya kuuza nyama wanapaswa kuvaa nguo stahiki na barakoa, hali ambayo kuna mwonekano wa kuendelea kupuuza kanuni hizo.

Dk. Yvonne Doyle, Mkurugenzi katika Wizara ya Afya, nchini Uingereza, anathibitisha kuarifiwa milipuko ya corona katika viwanda kadhaa vingine, vikiwamo vya kutengeneza nyama.

"Milipuko inapotokea, tunafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Afya kupima na kufuatilia waliopata maambukizi pamoja na kuhakikisha tunapata waliokaribiana nao, ndani na nje ya kampuni."

Nchini Ujerumani, serikali imeshapiga marufuku wafanyakazi kutoka nje,- badala yake wanaoruhusiwa ni wafanyakazi walioajiriwa na kampuni pekee.

Aidha, ripoti kutoka Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Marekani, imependekeza kupunguza kiwango cha uzalishaji na kuweka vizuizi vya kutenganisha watu.

Hapo inabeba maana kwamba, kuna kuvaa mkinga uso na kuhakikisha hakuna atakayekosa kulipwa, kwa sababu ya kujitenga.


Nchini Tanzania, bado ni ndani au kipindi cha wastani wiki moja tangu serikali kulegeza masharti ya kukabiliana na corona, hapo masomo yameanza kuendelezwa na baadhi ya shughuli za kijamii.

Hata hivyo umma unakumbushwa kuwa makini katika kutetea usalama wake na mazingira ya karibu kuendesha magari salama.



## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Utamaduni wa Mtanzania leo hii uko wapi?




**Na Joseph Kulangwa**



NA JOSEPH KULANGWA

WATANZANIA wanapenda sana utamaduni wao, hata kama ni kinadharia. Huridhika sana wanapotajwa duniani, kwamba wana utamaduni wao. Nao hujitapa sana kuwa wanadumisha utamaduni wao.

Hupenda sana kujitokeza hadharani na kujinasibu, kuwa na utamaduni wao na kuulinda. Hujinasibu katika nyimbo, ngoma na hata michezo. Hufikia hata kujigamba kuwa wana mavazi yao ya kitamaduni.

Hakuna taifa duniani lisilo na utamaduni wake, kwani utamaduni ni kielelezo cha uhai na utashi wa jamii. Lazima udumishwe.

Hivi ukimchukua Mtanzania, ukambwaga Nigeria bila kumtambulisha, kuna mtu atamtofautisha na Mnigeria kwa kumtazama tu? Hapana! Ni vigumu. Mpaka atambulishwe. Vinginevyo ataonekana ni Mnigeria tu.

Kuna vijana wawili wa Tanzania napenda tu kuwatumia kama mfano. Naseeb Abdul 'Diamond Platnumz' na Rajab Abdul 'Harmonize'. Hawa ni wasanii wa muziki wa kizazi kipya. Muziki wenye tabia ya kutungwa haraka haraka na kuimbwa au kupigwa huku ukigubikwa na maudhui ya kimapenzi zaidi.

Harmonize na Diamond ni 'pacha' katika muziki huu wa kizazi kipya. Diamond ni Kurwa na Harmonize ni Doto. Diamond akitangulia kutoka na Harmonize akifuatia, wakifanana karibu kwa kila kitu katika muziki huo. Si 'mistari' kama waitavyo wao tungo zao, mirindimo au cheza yao.

Wachukue pacha hao kutoka Tanzania na washushe ghafla Marekani na vivazi au mwonekano wao, hakuna atakayewatofautisha na Wamarekani weusi. Wachukue Wamasai wawili waliovaa lubega na kusokota nywele zao mtindo wa rasta, washushe hapo hapo, hakuna atakayejiuliza kuwa si Watanzania au Wakenya.

Utawala wa Awamu ya Tatu Tanzania, ulipata kuwa na Waziri Mkuu Frederick Sumaye, ambaye inakumbukwa, alipata kutoa msimamo kwamba ifanyikapo mikutano nchini ikihudhuriwa na Watanzania Waswahili wengi na Wazungu wachache, kitumike Kiswahili na hao wachache wafasiriwe. Alikuwa anakienzi Kiswahili.

Kama kawaida ikachukuliwa kinadharia. Mambo hayakubadilika. Awamu ya Tano ya Rais Dk John Magufuli, ikasisitiza kuwa sasa ni Kiswahili tu, ili kukienzi na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, lakini pia kukitangaza kimataifa. Imewezekana.

Si nadharia tena ni vitendo. Ubishi umebaki kwenye Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia vyuo vya juu. Tusubiri.

Miezi michache hivi karibuni, Harmonize alizindua albamu yake yenye nyimbo 18. Uzinduzi huo ukaitwa AfroEast2020. Ukumbi ukafurika wageni, wakiongozwana Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete.

Alikuwapo Waziri mwenye dhamana ya Utamaduni, Dk. Harrison Mwakyembe na Naibu Spika Dk. Tulia Ackson na wengineo wanaohusika na utamaduni na vijana. Ukumbi ulijaa pomoni.

Nilihudhuria kupitia matangazo ya televisheni. Hakika ilivutia kuangalia. Nilifuatilia kila kilichotokea, kuanzia kwa washereheshaji na utaratibu wa utambulisho wa nyimbo.

Waliotambulisha nyimbo niliwasikia baadhi wakitaja; 'Konde Boy For Every Body', 'Mama',` 'Never Give Up', 'Die', 'Wife', 'Malaika,' na zingine nyingi tu. Baadhi akishirikisha waimbaji nguli wa kimataifa kama vile Morgan Heritage, Khali Graph, The World na wengineo wakiwamo wa ndani kama Lady Jay Dee na Mr. Blue.

Nyimbo hizo karibu zote ziliimbwa kwa Kiingereza. Baadhi ya waliozungumza walimsifia Harmonize, kwamba anafanya vizuri katika muziki wake na anaitangaza Tanzania. Lakini, kina The World, Morgan na Graph wangeimba Kiswahili wakaenda kukitangaza kwao, ningeelewa dhana na dhima ya Harmonize kuitangaza Tanzania nje ya mipaka.

Harmonize kwa muktadha wa kibiashara anatafuta pesa, lakini kama ni kwa kuitangaza Tanzania kiutamaduni, sichelei kumlaumu. Anachokifanya yeye ndicho anachokifanya Kurwa. Mnigeria si Mnigeria, Mwafrika Kusini si Mwafrika Kusini, ili mradi muziki si wa kitanzania.

Nani alisema muziki wa kizazi kipya hauwezi kutangaza utamaduni wa Mtanzania? Nani alisema kuiga muziki wa kigeni wa Afrika Kusini, Nigeria au Marekani ndiko kuitangaza Tanzania nje ya mipaka? Tujinasibu kupiga muziki kutafuta ukwasi, lakini si 'kujimwambafai' eti tunaitangaza Tanzania nje ya mipaka. Alamsiki.

• Simu: +255 713 410008 na barua pepe:jkulangwa@yahoo.com

UCHUMI

# Nyenzo ya maendeleo Uhamiaji yatua Magu na makucha yake

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

IDARA ya Uhamiaji na majukumu yake, ni kiungo nyeti kufanikisha nyenzo za maendeleo kitaifa. Inaelezwa tija yake ina uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo kitaifa.

Ni moja ya sababu ambazo serikali iliyoko madarakani, inafanya huduma zake zifike kila mahali waliko wananchi na wakanufaika, kuanzia na usalama, huduma na mahitaji mengineyo ya kimaendeleo.

Hivi karibuni wilaya ya Magu mkoani Mwanza, ilinufaika kufunguliwa ofisi na Nipashe na ikaamua kuifanyia kazi, kwa kuongea na uongozu wa Uhamiaji mkoa kupata ufafanuzi wa majukumu na walivyojipanga, kusukuma mbele maendeleo hayo, kupitia majukumu walio nayo.

Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Bahati Mwaifuge, ambaye ni Ofisa Uhamiaji wa Mkoa wa Mwanza, anaeleza idara wanavyofanya kazi wilayani Magu, kuhakikisha usalama wake, ikiwamo udhibiti wa wahamiaji haramu.

Mkuu huyo wa Uhamiaji Mkoa, anasema wameongeza kasi ya kuboresha huduma katika wilaya za Mwanza, ikiwamo huduma mpya ya Magu. Ifuatayo ni mazunngumzo ya 'Ana kwa Ana' na Nipashe:



Ofisa Uhamiaji wa Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Bahati Mwaifuge, akiwa ofisini kwake. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

**SWALI: Ofisi ya Uhamiaji wilayani Magu, imeanzishwa lini?**

**JIBU:** Ofisi imeanzishwa Juni mwaka jana. Kabla ya hapo, maofisa wetu walikuwa wakienda kufanya kazi kutoka hapa mkoani, lakini tukaona tuanzishe ofisi zetu za Uhamiaji.

**SWALI: Madhumuni ya kuanzisha ofisi hizo ni nini hasa?**

**JIBU:** Lengo ni kuongeza huduma karibu na wananchi za Uhamiaji, kuongeza udhibiti wa wahamiaji haramu, kuongeza ulinzi na ushirikiano na vyombo vingine vya dola, kama vile Polisi, Magereza na jeshi la akiba(Washauri wa Mgambo), Takukuru pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

**SWALI: Uhamiaji wilayani humo inafanya kazi katika maeneo gani?**

**JIBU:** Idara yetu inafanya kazi katika maeneo yote ya mjini na vijijini, yaani ngazi ya kijiji na kata, kuhakikisha inapata taarifa kutoka kwa wananchi au raia wema za kuwepo wahamiaji haramu, pamoja na taarifa kutoka kwa viongozi wa ngazi hizo.

**SWALI: Je, Wahamiaji Haramu wengi wanapatikana katika maeneo yapi?**

**JIBU:** Maeneo yote ya mjini na vijijini wanapatikana. Tunakuwa tukifanya misako na maofisa wetu na kuwakamata, kisha tunawachukulia hatua, ikiwamo wengine kuwafikisha mahakamani.

> **"Tulianza kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji na kata ambao wamekuwa wakitoa taarifa katika ofisi yetu na wanawafichua wahamiaji haramu kwenye maeneo yao. Idara imekuwa ikichukua hatua za kuwakamata na kisha kuwafikisha mahakamani**

**SWALI: Tangu muanzishe ofisi hiyo Magu, mumefanikiwa kuwakamata wahamiaji haramu wangapi?**

**JIBU:** Tangu Juni mwaka 2019 tulipoanzisha ofisi yetu hadi Juni mwaka huu 2020, tumefanikiwa kuwakamata wahamiaji haramu 18. Kati yao, wawili wanatumikia kifungo, watu tisa tuliwarudisha kwao na watatu tuliwapa muda wa kurekebisha hadhi zao za kiuhamiaji.

Wengi wao tuliowakamata wanatokea nchi mbalimbali, ikiwemo raia watatu wa Kenya, Uganda mmoja, Burundi raia kumi, Zambia mmoja, Ethiopia wawili pamoja na India moja.

Lakini, tunapowahoji kwa nini wameingia nchini kinyemela, wanadai wamekuja kutafuta maisha na asilimia kubwa ni wale wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 40.

**SWALI: Sheria inasemaje kuhusu raia wa kigeni kuingia nchini hapa?**

**JIBU:** Anapokuja nchini, anatakiwa kuwa na pasipoti ya kusafiria na akiingia, lazima apewe kibali cha kuishi, vinginevyo kama hana vitu hivyo, huyo atakuwa ni mhamiaji haramu.

**SWALI: Hivi tafsiri ya mhamiaji haramu ni ipi?**

**JIBU:** Ni yule ambaye sio raia wa nchi hiyo, asiyepita kwenye njia rasmi. Pili, ni yule anayeingia kihalali nchini kwa kufuata sheria za uhamiaji, lakini kibali chake kikiisha na akaendelea kuishi, huyo tena anageuka kuwa mhamiaji haramu.

Jambo lingine ni kwamba, muda wake ukiisha anatakiwa kuondoka nchini, la sivyo anatakiwa kwenda mapema katika Idara ya Uhamiaji kutoa taarifa kama anataka kuendelea kuishi nchini, ili aweze kuongezewa muda lakini iwe kabla ya muda wake kwisha kabisa,

Pia, haitoshi kama mwenendo wake wa kuishi nchini humo haukuwa mzuri wa kuridhisha.

**SWALI: Je, wananchi wa Magu wamepata elimu ya kujua kuwafichua wahamiaji haramu.?**

**JIBU:** Tulianza kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji na kata ambao wamekuwa wakitoa taarifa katika ofisi yetu na wanawafichua wahamiaji haramu kwenye maeneo yao.

Idara imekuwa ikichukua hatua za kuwakamata na kisha kuwafikisha mahakamani,wengine kuwarudisha kwao, lakini wengi tukiwahoji wamekuwa wakidai amani hakuna kwenye nchi zao.

Vita, vurugu za kisiasa na maisha magumu ni moja ya chanzo cha kukimbia raia nchini mwao, lakini baadhi yao wanaona nchini Tanzania na kuna fursa nyingi za kujipatia kipato pamoja na amani tele,

**SWALI: Mikakati yenu ni ipi katika wilaya.?**

**JIBU:** Kwanza ni kutoa elimu kwa wananchi wote, ili kujua maana ya Uhamiaji haramu. Pili, kutoa elimu katika taasisi mbalimbali na mashirika ya umma, madhehebu ya dini na katika viwanda.

Tatu, kutoa elimu kwenye kampuni mbalimbali, 'NGO' (mashirika yasiyo ya kiserikali), shuleni na maeneo mengi ya kijamii, ili kila mmoja imfikie elimu hiyo. Lakini, sisi tunafanya doria, ukaguzi na misako kwenye vijiji na kata wilayani humo

**SWALI: Faida ni zipi kuhusu elimu hiyo?**

**JIBU:** Ni pamoja na wananchi hivi sasa wameanza kuelewa na kuanza kutoa taarifa kwenye ofisi zetu za idara wanapoona mgeni kijijini kwao wasiyemtambua au akitapatapa mitaani.

Lakini, faida nyingine ni wageni hivi sasa wanakwenda moja kwa moja kupata huduma za Uhamiaji katika ofisi ya wilaya, badala ya kulazimika kwenda hadi mkoani Mwanza.

Aidha, serikali nayo inaingiza kipato kutokana na faini wanazotozwa wahamiaji hao mahakamani, kulingana na makosa na wengine kutaifishwa mali wanazokuwa nazo,

Faida nyingine ni elimu ya uhamiaji inayotolewa kwa wananchi, itasaidia kupata uelewa wa masuala ya uhamiaji, ili nao wasiwe wahanga wa uhamiaji haramu katika mataifa mengine.

**SWALI: Madhara ya mhamiaji haramu ni yepi kwa jamii?**

**JIBU:** Akikaa miaka mingi nchini kwenye jamii, anaweza kupewa hata uongozi, kufanya matukio ya ujambazi, kuwanyonya huduma halali wananchi, mfano huduma za elimu, afya, maji na nyinginezo kutokana na kukosa uzalendo kwa vile sio nchi yake.

Aidha, kuingiza wahamiaji haramu wengine nchini bila kibali na kusababisha madhara au hasara kubwa kwa jamii na taifa kwa ujumla, kutokana na wao kutumia rasilimali za nchi zisizowahusu.



Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Magu, Mrakibu Salma Katongo.

**WITO WAKE**

Kamishna Msaidizi Mwaifuge, anatoa wito kwa wananchi waendelee kushirikiana na Idara ya Uhamiaji wilayani humo kuwafichukua wahamiaji haramu, pia kampuni, taasisi na mashirika ya umma yenye watumishi wageni, wawafikishe katika ofisi yao kupata huduma stahiki.

• ***Kwa mawasiliano: Simu +255 682 869244 na barupepe: anthonygervas@yahoo.com:***



# Mgonjwa wa 2 apandikizwa figo Hospitali Benjamin Mkapa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa imefanya upandikizaji wa figo kwa mara ya pili kwa kutumia madaktari wazawa bila kutegemea wa nje ya nchi.

Hatua hiyo imesaidia kuokoa gharama kubwa za matibabu nje ya nchi, ambapo mgonjwa mmoja hupandikizwa kwa Sh. milioni 100, ikiwa ni sawa na upandikizaji figo wa wagonjwa wanne hapa nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema mwaka 2018 hospitali hiyo ilianza kutoa huduma hiyo kwa kutegemea wataalamu kutoka Tokushukay Medical Corporation nchini Japan, wakishirikiana na wa hospitali hiyo na wengine kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

"Mafanikio ya utoaji huduma za kibingwa, katika serikali ya awamu ya tano tunashuhudia ndoto zikitimizwa kwa vitendo, mwaka 2018 tunapanga kuanza kupandikiza figo na ilipofika machi 2018 tulifanikisha kupandikiza mgonjwa wa kwanza ikiwa ni nje ya Dar es Salaam, lakini Machi 2020 ikiwa ni miaka miwili baadaye, tulifanya kwa mara ya kwanza kwa kutumia madaktari wazawa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema lengo lao lilikuwa ni kujifunza kutoka kwa wataalamu wa Japan ili kutoa huduma hiyo kama Watanzania.

"Leo nafuraha tena kuwajulisha kwa mara nyingine tumefanikisha kwa ufasaha mkubwa kupandikiza kwa mara ya pili mgonjwa kwa kutumia madaktari wazawa kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa na Chuo Kikuu cha Dodoma," alisema.

"Kweli kumbe Watanzania tunaweza, ilikuwa ni ndoto leo hii tumeweza, tunamshukuru Rais John Magufuli kwa kutujenga mtazamo wa kwamba kufanya mambo makubwa yanawezekana."

"Pia bado tunaendelea kutoa huduma nyingine za usafishaji damu na hadi sasa kuna wagonjwa 75 wamepata huduma hapa hospitali na kuna mashine ya uvunjaji mawe kwenye figo, wagonjwa 15 wamepata huduma," alisema.Aliwataka Watanzania kuwa na tabia ya kuchunguza afya ili kuziweka figo kuwa salama.

"Nitumie fursa hii kuwaasa Watanzania kuchunguza afya zao ili figo ziwe salama, na kuokoa fedha ambazo zingetumika kwa ajili ya matibabu zitumike kwa mambo mengine ya uwekezaji hapa nchini, tunashukuru serikali kwa kusikiliza mahitaji yetu na kutusaidia kwa kuwa imechangia kupata vifaa tiba vya hali ya juu na vya kisasa ambavyo vimewezesha kufikia hatua hii," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Figo na Daktari Bingwa, Dk. Kessy Shija, alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwasaidia Watanzania kuwa na uthubutu ambao umechangia kufikia hatua hiyo.

"Huduma ya upandikizaji wa figo ni ya kawaida, hivyo watu wenye shida mbalimbali za upandikizaji waje katika hospitali hii kwa kuwa ni huduma inayotolewa wakati wowote," alisema.

Alisema hadi sasa wagonjwa 13 wamepandikizwa figo na kati yao wawili na madaktari wazawa wanatoka maeneo mbalimbali ya nchi.

Naye, Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Ipyana Mwampagatwa, alipongeza timu ya wataalamu kwa kazi kubwa wanayoifanya na kuendelea kuimarisha huduma hiyo nchini.



Mwalimu Francis Mbisso kutoka Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa na watu wenye ulemavu kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo katika masuala ya uchaguzi, wakati wa warsha ya uboreshaji wa mazingira shirikishi na wezeshi kwa watu wenye ulemavu, iliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wenye ualbino: Msituue viungo vyetu haviwapi ushindi uchaguzi

**Renatha Msungu,** DODOMA

KUELEKEA uchaguzi mkuu, unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, watu wenye ualbino, wamekemea mauaji ya watu hao na kudai kuwa viungo vyao haviwezi kuwafanya wanasiasa kushinda katika nafasi za uongozi.

Wameiomba serikali kuweka mkazo katika tiba ya saratani ya ngozi pamoja na kuwateua katika nafasi za uamuzi watu wenye ulemavu. Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mwenyekiti wa Taasisi ya Foundation for Disabilities Hope, Michael Salali, wakati akitoa tamko la watu wenye ulemavu kuhusu kumpongeza Rais John Magufuli, kwa kutekeleza miradi mingi ya kimaendeleo.

Alisema wakati wa chaguzi miaka ya nyuma kulikuwa kuna wimbi la watu wenye ualbino kukatwa viungo vyao na baadhi ya wanaodaiwa kuwa ni wanasiasa.

Alisema serikali imetokomeza jambo hilo kwa kuwakamata wahusika wote.

"Kwa sasa tunashukuru vitendo vimepungua ila tuendelee kuiomba jamii kuepuka vitendo hivi na tunaiomba serikali ijayo iliangalie jambo hili kwa kuwa hiyo ni imani potofu," alisema. Pia, alisema wanaofikiri viungo hivyo vitawasaidia kushinda katika uchaguzi mwa Oktoba 2020, wanatakiwa kunadi sera zao na sio kukimbilia kwamba viungo vyao vitawasaidia kushinda. Alisema serikali ijayo iangalie mambo kadhaa kwa watu wenye ulemavu nchini ikiwamo kuweka mkazo katika tiba ya saratani ya ngozi. "Tunajua kwamba serikali ya awamu ya tano imefanya mambo mazuri katika sekta ya afya kwa kujenga vituo vya afya kila mahali, lakini tunaomba serikali ijayo ituangalie sisi hasa kwenye saratani ya ngozi kwani tumekuwa tukipata shida ya mionzi," alisema.

Vile vile alisema, wanaomba serikali ijayo iwakumbuke katika uteuzi wa nafasi za uamuzi kama ilivyofanya katika awamu ya tano kwa kumteua Balozi wa Ujerumani, Dk. Abdallah Possi na wengine.

Aliiomba serikali ijayo kusimamia mikopo ya asilimia mbili, inayotolewa na halmashauri nchini ili iwafikie watu wenye ulemavu.

Katika hatua nyingine, watu wenye ulemavu nchini wameipongeza serikali ya awamu ya tano kwa kutekeleza miradi mingi ya kimaendeleo ikiwamo ulinzi kwa watu wenye ulemavu wa ngozi. "Ulinzi wa watu wenye ulemavu hasa wenye ualbino umeongezeka na katika awamu hii ya tano, tumeshuhudia kupungua kwa vitendo vya ukatili ikiwamo kukatwa na kuchukuliwa viungo," alisema.

Salali, alisema wanampongeza Rais kwa kuchukua fomu ya kugombea urais kupitia CCM, kitendo hicho ni kiashiria cha imani ya wananchi juu ya utendaji wake uliotukuka. "Tunampongeza kwa kutoa fursa kwa wafanyabiashara wadogo katika stendi mpya ya mabasi ya Dodoma hii ni fursa adhimu kwetu kwa watu wenye ulemavu pamoja na watu wenye kipato cha hali ya chini," alisema.

# Sekta umwagiliaji kufikisha hekta mil. 1

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), imeweka mikakati mbalimbali itakayowezesha kufikia azma ya taifa ya kuendeleza sekta ya umwagiliaji ili kufikia hekta milioni moja ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hiyo, Daudi Kaali, alisema wamepanga kutekeleza mikakati hiyo ili kufikia azma hiyo ifikapo mwaka 2025.

Alisema, moja ya mkakati ni kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji, Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4, ya mwaka 2013, kifungu cha 52 (1) inaeleza kuanzishwa kwa mfuko huo ili kuwa na maendeleo endelevu katika sekta hiyo.

"Utekelezaji wa sheria ya mfuko wa maendeleo ya umwagiliaji utaiwezesha Tume kuongeza ufanisi, katika utekelezaji majukumu yake ya kila siku ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mitambo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na jumla ya Sh. bilioni 300.4 zimekadiriwa kukusanywa katika kipindi cha miaka mitano," alisema Kaali.

Pia, alisema mkakati mwingine ni kuanzisha kampuni ya ushauri na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, na mpaka sasa Tume, imekamilisha taratibu za kusajili kampuni ya ushauri wa miuondombinu ya umwagiliaji. Alisema, Tume ipo katika mchakato wa kuanzisha kampuni tanzu ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, hatua ambayo itasaidia kupunguza gharama za ujenzi na kuimarisha ubora wa miundombinu ya umwagiliaji.

Kadhalika, alisema mikakati mingine ni kutekeleza miradi ya kimkakati ya umwagiliaji ikiwamo kuendeleza Bonde la Mto Ruvuma hekta 26,066, Mto Ruhuhu hekta 3,700, Mto Songwe hekta 3,005, Mto Rufiji hekta 64,896 na Mto Luiche hekta 3,000.

"Pia kutekeleza mpango wa ujenzi wa mabwawa maeneo kame nchini kwa ajili ya kilimo ya umwagiliaji, hii ni moja ya vipaumbele vya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kutokana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kutokana na miradi mingi kukabiliwa na changamoto ya uhaba wa maji na vyanzo vingi vya mito kukauka," alisema Kaali.

Alisema ili kutatua changamoto hiyo Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imepanga kujenga mabwawa yatakayotumika kwenye kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine.





# Kyela waanza ujenzi wa shule mbili za kata

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAKAZI wa Kata ya Busale Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya wameamua kuanzisha ujenzi wa shule mbili mpya za sekondari.

Lengo la mpango huo ni kuondokana na tatizo la mrundikano wa wananchi katika Shule ya Sekondari ya kata hiyo ya Kiwira Coal Mine KCM.

Wakizungumza jana na Nipashe wakazi hao, walisema walikubaliana kuchanga kiasi cha fedha kuanzia shilingi 10,000 kwa kila kaya pamoja na nguvu kazi ili kukamilisha ujenzi huo.

Kata hiyo yenye jumla ya vijiji vitano na wakazi zaidi ya 6,000 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 waliamua kuanza ujenzi wa shule mbili za sekondari, ili kupunguza mrundikano na kuwasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu.

Miongoni mwa wakazi hao akiwamo Japhet Mwakitubwa alisema licha ya kuwapo na mrundikano wa wanafunzi katika darasa moja, lakini kumekuwapo na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaofaulu kujiunga kidato cha kwanza na kupelekwa Sekondari ya KCM.

Kutokana na sababu hizo kwa pamoja walikubaliana kuanza ujenzi wa shule nyingine ya sekondari ambayo itasaidia kupunguza idadi ya wanafunzi kwa shule moja.

Joachim Mwandemele ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Ikomelo alisema licha ya kuanza ujenzi wa shule mbili mpya za sekondari ambayo umefikia hatua ya mtambaa wa panya, lakini walikubaliana kumejenga madarasa manne kwa ajili ya kuanzisha kidato tano na cha sita katika Shule ya Sekondari KCM.

Akizungumzia hatua hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, aliwapongeza wananchi kwa uamuzi huo na kutambua vikwazo vinavyowakabili wanafunzi na kuamua kujenga shule zingine.

Alisema serikali inaendelea na utaratibu wa kuongeza nguvu kwa kuwashirikisha wadau wengine ili kwa pamoja waweze kukamilisha ujenzi wa shule hizo ambao utawasaidia watoto kusoma kwa utulivu.

# Mwalimu adaiwa kumwibia mwenzake mamilioni benki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya linamshikilia mwalimu wa Shule ya Msingi Mwakaleli iliyoko Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, Joseph Shila (29) kwa tuhuma za wizi wa fedha.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kuiba kiasi cha shilingi milioni 34 ambazo ni za mwalimu mstaafu, Gideon Mwalujobo (60), mkazi wa Mwakaleli.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, mtuhumiwa alikamatwa Juni 30, mwaka huu majira ya usiku katika Kijiji cha Mwakaleli baada ya kupata taarifa za siri kutoka kwa wasamaria wema.

Taarifa hizo kutoka kwa wasamaria wema zilieleza kuwa mtuhumiwa alifanikiwa kuiba fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 34 mali ya mwalimu mstaafu Mwalujobo.

Matei alisema mtuhumiwa alifanikiwa kuiba kupitia akaunti namba 6140201871 kwa kutumia "NMB Mobile" katika Tawi la NMB Mbalizi Road, baada ya kupata namba ya siri ya mwathirika ambaye walikuwa ni walimu wa shule moja na marafiki wa siku nyingi.

Aidha, Matei alisema kuwa mtuhumiwa pia anajihusisha na uwakala wa kusajili laini za simu kwa kutumia mfumo wa kisasa wa alama za vidole.

Kamanda Matei alieleza zaidi kuwa mtuhumiwa huyo alitengeneza laini ya simu kwa jina la Mhanga na kutokana na kuaminiana na muathirika, pia alikuwa ana mpa kadi yake ya benki kwa ajili ya kumtolea fedha.

Kwa mujibu wa Matei, katika upekuzi uliofanywa nyumbani kwa mtuhumiwa, alikutwa na fedha taslimu shilingi 20,780,000, kadi ya benki ya NMB, simu tatu na laini mbili za simu.

Mara baada ya mtuhumiwa kutiwa nguvuni Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi wa shauri hilo baada ya kukamilika atafikishwa mahakamani.

"Natoa wito kwa wananchi kuwa makini na kadi zenu za benki ikiwa ni pamoja na kuhakikisha unatunza namba ya siri ili kujiepusha na matukio ya wizi," alisema na kuongeza:

"Lakini vilevile mwendelee kuhakiki usajili wa laini kwa kubonyeza *106# chagua 2, kisha ingiza nambari ya kitambulisho chako cha NIDA utapata kujua kitambulisho chako kimetumika kusajili laini ngapi.

"Na endapo kuna dosari zozote ni vyema kutoa taarifa mapema katika mamlaka husika kwa hatua zaidi."




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akionyesha fedha taslimu Sh. milioni 20, kwa waandishi wa habari, jijini Mbeya jana, zilizookolewa na jeshi hilo kati ya milioni 34 za Mwalimu mstaafu, Gideon Mwakalujobo zonazodaiwa kuibwa na a Joseph Shila (hayupo pichani) wa Shule ya Msingi Mwakaleli. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Bil. 20/- kupanua uwanja wa ndege

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetenga kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuanza upanuzi na ufungaji wa taa kuzunguka eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), ili kuruhusu ndege kubwa za mizigo na za masafa marefu kutua uwanja muda wowote.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati alipozungumza na wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa lengo la kuwaeleza masuala mbalimbali yaliyofanywa na serikali katika kuwahudumia.

Alisema Uwanja wa Ndege wa Songwe pamoja na kwamba umekamilika, lakini bado una mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa taa za kuongezea ndege nyakati za usiku, hali inayosababisha baadhi ya watu hususani wafanyabiashara kushindwa kusafiri kufuata bidhaa zao.

"Moja ya mikakati wa serikali kwa sasa ni kuuboresha uwanja huo, ambapo shilingi bilioni 20 zilitolewa ili kuanza ujenzi wa upanuzi na ufungaji wa taa kuzunguka eneo la uwanja, ili kuruhusu ndege kubwa za mizigo kutua pamoja na kutoa fursa wakulima na wafanyabiashara kusafirisha mazao yao kwenda nje ya nchi," alisema Chalamila.

Mmoja wa wakulima wa Wilaya ya Mbeya, Lupakisyo Mwakitalu, alisema kupanuliwa kwa uwanja huo kutakuwa ni mwarobaini wa soko la pareto, maharage na mahindi.

Alisema kutokana na jitihada zilizofanywa na serikali za ununuzi wa ndege kwa sasa gharama za usafiri zimekuwa nafuu ukilinganisha na ilivyokuwa awali, lakini ni usafiri ambao hutumia muda mfupi, hivyo unafaa kwa ajili ya shughuli za kujiingizia kipato.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini maarufu ikiwamo Mbeya, inasifika kuwa na hali ya hewa nzuri na ardhi yenye rutuba inayostawisha kwingi mazao aina ya matunda, mboga na maua, hivyo uwapo wa uwanja huo wa ndege ni msaada kwao kwani wanautumia kusafirisha mazao hayo kuyauza.





Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud (kulia), akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, kuhusu ugawaji wa majimbo Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Balozi Iddi ataja sifa mgombea CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya CCM, Balozi Seif Ali Iddi (pichani), amesema mgombea atakayeteuliwa kupeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, atapaswa kuungwa mkono kwa asilimia kubwa na wanachama wote ili apate nguvu ya kushinda na hatimaye kushika dola Tanzania na Zanzibar.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa na wajumbe wa Mabaraza ya Jumuiya za CCM wa Mkoa Kaskazini Pemba katika ukumbi wa Chama, Micheweni.



Alisema watangaza nia ya urais wa Zanzibar kupitia CCM ni wengi, lakini anayetakiwa ni mmoja na akishapatikana kupitia mchakato wa upembuzi, lazima aungwe mkono na makundi yote yaliyosimama kuomba nafasi hiyo kwa upande wa Zanzibar.

Katika kumpata mwana CCM mahiri na mzalendo anayeuzika kwa wananchi, alisema viongozi watakaohusika katika uteuzi huo waelewe kwamba wanabeba dhima kuhakikisha watakayemteua ana sifa hasa kwa upande wa Zanzibar.

"Mgombea atakayefanikiwa kupata ridhaa ya wananchi walio wengi atakuwa na kazi ya kubeba dhima ya kusimamia maendeleo ya Taifa na kustawisha Maisha ya Umma," alisema.

Kuhusu ubunge, uwakilishi na udiwani, Balozi Iddi alisema viongozi na wananchi wa majimbo, ndio wanaowaelewa kwa kina watu wenye sifa za kujitolea katika kuwatumikia wananchi.

Balozi Iddi alisema wanachama wanaopewa jukumu la kuwatumikia wananchi na baadaye kuhamia kimaisha katika maeneo mengine hawafai na wapigakura lazima wajihadhari na watu wenye tabia hiyo.

Alisema viongozi wanaokabidhiwa dhamana ya kuwatumia wananchi lazima wajielewe kwamba ni watumishi wa wananchi na si watawala kama baadhi yao wanavyofikiria katika akili zao kwa vile walitumia rushwa katika kupata nafasi hizo.

"Kiongozi hatakiwi kwa fedha zake bali apewe dhamana kwa mujibu wa uzalendo wake unaompa nguvu za kuwatumikia wananchi katika eneo lake la utumishi," alisema.

Katika hatua nyingine, Balozi Iddi ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, aliwapongeza viongozi na wananchi Kisiwani Pemba kwa umahiri wao uliowezesha kisiwa hicho kuwa salama na wimbi la maambukizo ya virusi vya corona.

Alisema kitendo cha viongozi na wananchi kufuata miongozo ya wataalamu wa afya, ndicho kilichowapunguzia hofu na kujikuta wakiendelea na harakati zao za kimaisha bila wasiwasi wowote.

# Atangaza nia kuboresha afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassani Ameir, ametangaza nia ya kugombea urais wa Zanzibar, huku akijinadi kuboresha afya endapo atachaguliwa.

Akizungumza baada ya kutangaza nia, Ameir alisema hivyo ndivyo vipaumbele vyake iwapo atapata ridhaa hiyo kupitia chama chake na kushinda uchaguzi.

"Vipaumbele vyangu ni vingi sana, lakini endapo nitachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, naahidi kuboresha elimu hasa sayansi na teknolojia pamoja na afya bure kwa Wazanzibari wote," alisema. Pia alisema ataboresha huduma zote muhimu kwa wananchi kama vile majisafi na salama na kusema huduma zote zitakuwa ni bure.

Aidha, alisema atahakikisha anakuza utalii wa Zanzibar wenye tija kwa wananchi wote na kuzalisha ajira nyingi kwa vijana na kukuza pato la taifa na pato la mtu mmoja mmoja kupitia sekta hiyo. "Endapo nitachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, huduma muhimu kama vile majisafi na salama itakuwa bure. Lakini nitahakikisha utalii katika visiwa hivi unawanufaisha Wazanzibari kwa kuzalisha ajira nyingi," alisisitiza.

Katibu Mkuu huyo alisema atahakikisha Zanzibar inajengeka kimiundombinu na kujengwa kwa viwanda vikubwa na vidogo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuzalisha ajira kwa vijana.

# Serikali yaahidi wakulima neema

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuwapatia wakulima pembejeo kwa wakati kuhakikisha kilimo cha mpunga kinaleta tija kwa manufaa ya taifa.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kuangalia uvunaji wa mpunga Upenja Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema malengo makuu ya serikali ni kuwasaidia wakulima kuwapatia pembejeo zote za kilimo ili kuzalisha mazao kwa wingi. Dk. Makame alisema serikali inatazama kwa makini suala la kilimo na kushajihisha wakulima ili kuona tija inapatikana kwao na serikali kwa ujumla.

Kutokana na uvunaji huo, aliwapongeza wakulima kwa mavuno mazuri licha ya kwamba wakulima wengi walikata tamaa katika kipindi cha mvua kutokana na mashamba yao kujaa maji.

Aliwaomba wakulima kutokata tamaa yanapotokea mabadiliko ya tabia nchi na badala yake kulima kwa wakati kama walivyozoea kwa kuwa kilimo kinalipa.

"Kilimo kinalipa. Ni muhimu wakulima kulima, kupanda, kupalilia na kupanda mbegu bora na kuvuna kwa wakati. Wasichukue mbegu ambazo hazina mapato makubwa kwani mbegu bora ndizo zitakazowasaidia," alisema.

Dk. Makame pia aliwashauri wakulima kulima kwa kutumia utaalamu kwa ajili ya kuendeleza kazi yao na kutopinga maelekezo wanayopatiwa kwa kuwa ni faida yao na badala yake kushirikiana na wizara ili kuendeleza kilimo chao.

"Tukishirikana pamoja katika kilimo basi Zanzibar itajitocheleza kwa chakula cha aina yoyote ikiwamo mpunga," alisema.

Aliwataka mabibi shamba na mabwana shamba kushirikiana na wakulima kwa kukaa nao karibu ili waweze kulima kwa mfumo ambao utawaletea tija.

Nao wakulima hao walisema pamoja na hali ya hewa kuwa ngumu, baadhi yao walilima na kupata mavuno mazuri. Mmoja wa wakulima hao, Amour Saleh Furaha, aliiomba serikali kuendelea kuwapatia pembejeo kwa muda ili kuendana na hali ya hewa na kilimo chao.

Alisema iwapo serikali itawarahishia miundombinu na kuwapatia pembejeo mapema basi itawasaidia kupata mazao ya kutosha na kuongeza kipato.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NATAFUTA KAZI YA UDEREVA NA SALES,** MIMI IRENE J. BWIRE MWENYE UMRI WA MIAKA 28 NATAFUTA KAZI YA UDEREVA NA SALES. UZOEFU WANGU NI MIAKA 8 SASA. KWA MAWASILIANO NIPIGIE KWA SIMU NAMBA 0689 617313.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI

**Colin Sambwe** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba T678 ARB aina ya ISUZU iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/MAG/RB/498795/2020**

157969

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;173/2020**

Ombi la **SELINA TAUSI PEREKA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu APPOLINARIA ELIKANA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/07/2020.

157978

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHEILA ALLY JUMANNE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 728 DJG TOYOTA NOAH.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya Polisi: DAR/URA/RB/495384/2020**

157975

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILBAD SEREYA WILBAD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 940 CED TOYOTA HILUX. Chassis namba RZN1470021034. Engine namba IRZ2392565.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: KIL/HAI/RB/565242/2019.

157974

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**SONGEA DISTRICT REGISTRY**
**AT SONGEA**

**Rule 13, Subordinate Court (Civil Procedure)**

**CIVIL CASE NO. 06 OF 2019**

**NMB BANK PLC.............................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF MVIWAMBI FARMERS GROUP 1ST DEFENDANT**
**MEINRAND JOHN NCHIMBI ............................2ND DEFENDANT**
**PHILEMON INNOCENT MA.................................3RD DEFENDANT**
**KASIAN ALOYCE MAPUNDA...............................4TH DEFENDANT**
**BUNUS HYERA.........................................................5TH DEFENDANT**
**AGATON JOSEPH MBEPERA ..............................6TH DEFENDANT**
**IMMACULATE JOHN NDUNGUR..........................7TH DEFENDANT**
**KASSIAN MAPUNDA ..............................................8TH DEFENDANT**
**CLEMENCE LEMBERE..............................................9TH DEFENDANT**

**TAKE NOTICE THAT:** the plaintiff has instituted a suit you with particulars of claims set out in the amended plaint filed in this court. Service of the summons to you has been ordered by means of publication. You are hereby summoned to appear in this court in person or by an advocate or by an agent duly authorized on 9th 2020 at 9:00 a.m when this suit will be mentioned.
**TAKE FURTHER NOTICE** that should you default enter appearance in court on the day and time mentioned above the suit will proceed may be given in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 2nd day of June 2020

115798602

---

## KUPOTEA KWA KADI

**Farayi Lovejoy Masuka** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba T562 AEY aina ya SURF iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/MAG/RB/498795/2020**

157968

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
wilaya ya DODOMA

MADAI NAMBARI 39/2020
MDAI .......... SCOLASTICA DAUD MLILA
MDAIWA............ELIKANA CHARLES SHIRIKALE

KWA... ELIKANA CHARLES SHIRIKALE

Kwa Kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
ANADAI TALAKA

Hivyo unahitajika /mnahitajika kuhudhurua binafsi katika Mahakama hii siku jumanne tarehe 14/7/2020 saa 02:30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 01/7/2020

157984

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DIPESH CHANDRAKANT KANSARA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 635 BYG** TOYOTA RANGI YA MAROON. Chassis namba **SXM100138498.** Engine namba **352738498.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **TAN/RB/498641/2020.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HILARY JOACKIM KINJO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 844 AGH** aina ya Toyota **RAVA 4** rangi Nyeupe.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/484745/2020.**

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**SONGEA DISTRICT REGISTRY**
**AT SONGEA**

**Rule 13, Subordinate Court (Civil Procedure)**

**CIVIL CASE NO. 06 OF 2019**

**NMB BANK PLC.............................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**GIBO BEATUS LEMBELE....................................10TH DEFENDANT**
**PHILO NDUNGURU...........................................11TH DEFENDANT**
**SAMWEL NDUNGURU.......................................12TH DEFENDANT**
**REMIGIUS KAPINGA........................................13TH DEFENDANT**
**AROIS KASSIAN MAPUNDA.............................14TH DEFENDANT**
**AMOS BLASTUS MAPUNDA.............................15TH DEFENDANT**
**DESTERIUS MAPUNDA......................................16TH DEFENDANT**
**ISACK KINUNDA ...............................................17TH DEFENDANT**
**TEOFORD KAPINGA...........................................18TH DEFENDANT**

**TAKE NOTICE THAT:** the plaintiff has instituted a suit you with particulars of claims set out in the amended plaint filed in this court. Service of the summons to you has been ordered by means of publication. You are hereby summoned to appear in this court in person or by an advocate or by an agent duly authorized on 9th July,2020 at 9:00 a.m when this suit will be mentioned.
**TAKE FURTHER NOTICE :**that should you default enter appearance in court on the day and time mentioned above the suit will proceed may be given in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 2nd day of June 2020

115798302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;169/2020**

Ombi la **VICTORIA MICHAEL BENGESI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **KISHALULI JOSEPH KISHALULI** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/07/2020.

157971

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;172/2020**

Ombi la CATHERINE BERNARD MINJA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ELEUTERI SIMON NGOWI Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/07/2020.

157972

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO.**
**SHAURI LA MADAI NA.22 YA 2018**

**MARGARETH SARAMAKI STEPHEN............MSHINDI TUZO.**

**DHIDI YA**

**BENROSE TANZANIA LIMITED...........MSHINDWA TUZO**

**NOTISI YA KUSIKILIZWA**

KWA: BENROSE TANZANIA LIMITED

NOTISI hii ni ya kesi tajwa hapo juu,ambayo imepangwa kusikilizwa utekelezaji tarehe 23 mwezi wa 7 mwaka 2020 Saa 2:30 asubuhi mbele ya mahakama ya hakimu mkazi Morogoro.

Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili au mtu yeyote aliyeidhinishwa kusimama kwa niaba yako na pia unatakiwa kutoa siku hiyo nakala zote za ushahidiutakazotumia katika utekelezaji Wake

Zingatia kwamba,Kutoudhuria siku ya kesi na wakati uliotajwa hapo juu,.Mahakama itaendelea na kuikiza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako

Imetolewa chini ya muhuri wa mahakama leo tarehe
Siku ya tarehe 30 mwezi 06 mwaka 2020.

157965

**Uza,**

**Chenye Thamani**

**Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MATANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imetoa adhabu kwa makampuni ya simu yafuatayo: **Airtel Tanzania Plc, MIC Tanzania Plc, Smile Communications Tanzania Ltd, Tanzania Telecommunications Cooperation, Viettel Tanzania Plc, Vodacom Tanzania Plc, na Zanzibar Telecoms Plc** kwa kutakiwa kulipa faini mbalimbali kutokana na makosa ya kutoweka vigezo na masharti sahihi, kwenye vifurushi, na bidhaa au huduma watoazo.

Hatua hii imefikiwa na TCRA baada ya kubaini kuwa makampuni tajwa ya Simu wamekuwa walikiuka Kanuni Na. 4 & 7(3) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ulinzi kwa Mlaji), 2018 na Kanuni Na. 12(4) ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ushuru/tozo), 2018 pamoja na kutozingatia maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na TCRA.

Baada ya kubainika kwa ukiukwaji wa Kanuni hizo na kwa mujibu wa Kifungu cha 48 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Sura ya 172 marejeo ya 2017 ya Sheria za Tanzania, makampuni hayo; **Airtel Tanzania Plc, Zanzibar Telecoms Plc, Viettel Tanzania Plc, MIC Tanzania Plc walitakiwa kufika mbele ya TCRA tarehe 11 Juni 2020 ilhali Vodacom Tanzania Plc, Tanzania Telecommunications Cooperation na Smile Communications Tanzania Ltd** walifika **tarehe 12 Juni, 2020,** ili kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria na kikanuni kwa ukiukaji huo wa Kanuni. Makampuni hayo yalifika mbele ya TCRA kama yalivyoamriwa.

Baada ya TCRA kuzingatia utetezi uliotolewa na makampuni yote tajwa hapo juu na kujiridhisha kuwa ni bayana yamekiuka Kanuni, na kwa mujibu wa Kifungu cha 48 (2)&(3) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 marejeo ya 2017 ya Sheria za Tanzania, TCRA imetoa adhabu kwa makampuni hayo kama ifuatavyo: -

**A. Airtel Tanzania Plc**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **350,000,000/=** (Milioni Mia Tatu na Hamsini), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

**B. MIC Tanzania Plc**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **300,000,000/=** (Milioni Mia Tatu), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

**C. Smile Communications Tanzania Ltd**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **15,000,000/=** (Milioni Kumi na Tano), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

**D. Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **30,000,000/=** (Milioni Thelathini), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

**E. Viettel Tanzania Plc**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **130,000,000/=** (Milioni Mia Moja Thelathini), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

**F. Vodacom Tanzania Plc**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **400,000,000/=** (Milioni Mia Nne), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

**G. Zanzibar Telecoms Plc (ZANTEL)**
1) Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) faini ya Shilingi **25,000,000/=** (Milioni Ishirini na Tano), tu.
2) Kutakiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kutoa taarifa kwa TCRA namna walivyo ya shughulikia kabla ya tarehe **30 Julai, 2020;**

Iwapo Makampuni hayo yatashindwa kutekeleza maagizo haya, TCRA itachukua hatua zaidi za kiudhibiti na kisheria pasipo kutoa taarifa zaidi na kwa gharama zao wenyewe.

**IMETOLEWA NA**

**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**2 Julai, 2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### UAMUZI WA SHAURI LA UKIUKAJI WA KANUNI ZA UTANGAZAJI DHIDI YA VITUO VYA CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO, EAST AFRICA RADIO, DUMA TV, GLOBAL TV, SIBUKA TV NA STAR TELEVISION

**1.0 Utangulizi**
Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano leo imetoa uamuzi dhidi ya vituo vya utangazaji vya **CLOUDS ENTERTAINMENT FM RADIO, DUMA TV, EAST AFRICA RADIO, GLOBAL TV, SIBUKA TV NA STAR TELEVISION** kwa kukiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018 na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

**2.0 Uamuzi**

**2.1 Clouds Entertainment FM Radio**
Kituo cha Clouds Entertainment FM Radio cha Dar es Salaam kimepatikana na hatia ya kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji kwa kurusha maudhui yenye kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono na utumiaji wa supu ya pweza katika kuimarisha tendo la ndoa katika muda ambao wasikilizaji wanaweza kuwa watoto. Kituo kimekiuka Kanuni Na. 11 (c); 12(1) (a), (d), na 14 (a), (b) na (c) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018

Kamati ya maudhui imetoa Uamuzi wake dhidi ya Clouds Entertainment kama ifuatavyo:-
a) Wanapewa Onyo Kali pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha na kurudia makosa kama hayo;
b) Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

**2.2 Duma TV**
Kituo cha Duma TV cha Dar es Salaam kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram, kimepatikana na hatia ya kukiuka Kanuni kwa kuchapisha na kutangaza maudhui yenye lugha isiyo na staha na yenye udhalilishaji wa kijinsia kwa wanaume na wanawake . Aidha, kupitia mtandao wao wa Instagram Duma TV waliongea maneno yasiyo na staha kwamba Waislamu wengi wanapenda wanawake wenye mashepu (maumbile) na kuwafananisha wanaume wenye udhaifu katika matamanio kwamba ni sawa na maiti. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 7(1) (a) na (b) na 12 (k) (i) (ii) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

Kamati ya Maudhui imetoa Uamuzi wake dhidi ya Duma TV kama ifuatavyo:-
a) Wanapewa Onyo Kali,
b) Wamefungiwa kuchapisha maudhui kwa muda wa mwezi mmoja ili wajipange na kuzifahamu vizuri Kanuni na kuzingatia weledi na maadili ya utangazaji.
c) Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Saba (TZS. 7,000,000.00)** tu, itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA

**2.3 East Africa Radio**
Kituo cha East Africa Radio kimepatikana na hatia ya kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya utangazaji kwa kurusha maudhui yenye kukashifu utendaji wa Serikali katika uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, vilevile kutumia lugha ya kashifa dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwamba hana meno katika utendaji wake wa kazi Kinyume na Kanuni Na. 17 (1); 24 (a), (b), (c), na 29 (b) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018;

Uamuzi dhidi ya Kituo cha East Africa Radio ni kama ifuatavyo:-
a) Wanapewa Onyo Kali;
b) Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tatu (TZS. 3,00,000.00)** tu itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

**2.4 Global TV**
Kituo cha Global Online TV cha Dar es Salaam kupitia chaneli yake ya Youtube kimepatikana na hatia ya kuchapisha picha za mnato na kutangaza maudhui yasiyo na lugha ya staha na yenye kushabikia vitendo vya mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja. Vile vile Maudhui yanayoweza kuwaumiza na kuwakwaza waumini wa dhehebu la Anglikana na jamii ya Kitanzania kwa ujumla, jambo ambalo ni kinyume na Sheria,Kanuni na Maadili ya Utangazaji. Global Online TV wamekiuka Kanuni Na. 5(1) (a) na (b), 7(1) (a) na (b) na 12 (b) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

Kamati ya Maudhui imetoa Uamuzi wake dhidi ya Global Online TV kama ifuatavyo:-
a) Wanapewa Onyo Kali;
b) Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Saba (TZS. 7,000,000.00)** tu itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

**2.5 Sibuka Television**
Kituo cha Sibuka Television cha Dar es Salaam kimepatikana na hatia ya kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji kwa kurusha maudhui yasiyo na staha na yenye kushabikia vitendo vya mauaji ya kutisha katika muda ambao watoto wanaweza kuwa sehemu kubwa ya watazamaji na hivyo maudhui hayo yanaweza kusababisha adhali za akili kutokana na hofu na woga wanaoweza kupata kwa kutazama maudhui hayo ya kutisha. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 5 (f) (g); 11(2) (c) ; 12(1) (a), (b), (d); 13(a) (b) (i) (ii) (iii) (iv) (ix) ; 14 (a (b) na 38 (1)(2) (3) (c) (d) ; 38 (4) (a) (b) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

Kamati ya Maudhui imetoa Uamuzi wake dhidi ya Sibuka Television kama ifuatavyo:-
a) Wanapewa Onyo,
b) Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tatu (TZS. 3,000,000.00)** tu itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA );

**2.6 Star Televiion**
Kituo cha Star Television cha Mwanza kimepatikana na hatia ya kukiuka Kanuni na Maadili ya Utangazaji kwa kurusha maudhui ya kukashifu viongozi wa Wilaya ya Kisarawe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mhe. Selemani Jafo (MB) kinyume na Kanuni Na. 11 (1)(f), 15(2)(b), 15(2)(c) na 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

Kamati ya Maudhui imetoa Uamuzi wake dhidi ya Star Television kama ifuatavyo:-
a) Wanapewa Onyo Kali;
b) Wanatakiwa kuomba radhi kwa siku tatu (3) mfululizo kwa wasikilizaji wao ambao waliathirika na maudhui yao, kupitia kipindi kilichotumika kutendea makosa.
c) Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00) tu** itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

**Taarifa hii imetolewa na:**
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Maudhui**
**01/Julai/2020**

## HABARI MICHEZO



# KLOPP
## AAHIDI KUTETEA TAJI EPL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema msimu ujao watatumia mbinu za kibabe, ili kutetea ubingwa huo kwa kishindo.

Mabingwa hao wapya wa Ligi Kuu England walifanikiwa kutwaa taji hilo wiki iliyopita, wakisaliwa na michezo saba mkononi, huku wakifanya hivyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30 kupita.

Mara ya mwisho kwa Majogoo hao wa Anfield kutwaa ubingwa wa England (Ligi Daraja La Kwanza kwa wakati huo) ilikuwa mwaka 1990.

Klopp, aliyejiunga na Liverpool mwaka 2015 akitokea Borrusia Dortmund, amesema lengo kuu la klabu hiyo ni kuhakikisha taji la EPL linasalia Anfield, na ana uhakika kazi hiyo itafanikiwa kutokana na kikosi imara atakachokitengeneza baada ya msimu huu.

"Hatutatetea taji msimu ujao, bali tutaushambulia ubingwa kuhakikisha tunaupata, tena kwa kishindo kikubwa," alisema Klopp.

"Nimejifunza kitu kwenye ligi hii unapojiona umeshinda basi ndiyo mwanzo wa kushuka kwani kila timu iko vizuri." Alisema meneja huyo kutoka Ujerumani.

Liverpool wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu England kwa tofauti ya alama 23 dhidi ya timu inayoshika nafasi ya pili, Manchester City.

# SAKA AONGEZA MKATABA ARSENAL

**LONDON, England**

NYOTA wa Arsenal, Bukayo Saka amesema kuwa anafurahi kuongeza mkataba ndani ya klabu hiyo kwa kuwa ni nyumbani na anapenda kuendelea kubaki hapo.

Ripoti zinaeleza kuwa Arsenal wamempa dili refu nyota huyo huku miaka aliyoongeza ikiwekwa kibindoni ili abakie ndani ya kikosi hicho.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 18 yupo tayari kuendelea kukipiga ndani ya kikosi hicho kilicho chini ya Kocha Mkuu, Mikel Arteta.

Kabla ya kuongeza dili jipya nyota huyo alikuwa anawindwa na Liverpool, Manchester United pamoja na Bayern Munich.

Arteta amesema kila siku nyota huyo amekuwa bora kila wakati ndani ya uwanja na hivyo asingependa kuona anaondoka.

Mchezaji huyo amekuwa na wakati mzuri zaidi kila anapopewa nafasi ya kucheza kwenye kikosi hicho msimu huu.




# DI MARIA AITAJA BARCELONA

**PARIS, Ufaransa**

KIUNGO wa PSG, Angel Di Maria amesema kuwa Barcelona walitaka kumsajili mwaka 2017, lakini alikataa.

Ubora wa kiungo huyo raia wa Argentina umezivutia timu nyingi ambazo zinahaha kupata saini yake ikiwa ni pamoja na Barcelona.

Di Maria amesema kuwa Barcelona walimfuata mwaka 2017 ila aligoma kusaini dili lao kwa sababu PSG ilikataa kumruhusu.

"Barca walijaribu kunisajili lakini mwisho wa siku klabu zote zilijadili na PSG ikagoma kuniruhusu kuondoka," amesema Di Maria akinukuliwa na gazeti la AS.

Amesema yeye hakuwa na kipingamizi cha kwenda kucheza kwa miamba hao wa pale Katalunya, lakini waajiri wake walionyesha nia ya kuendelea kumhitaji na hivyo akalazimika kubakia na timu hiyo.

Nyota huyo ambaye amewahi kukipiga Manchester United na kushindwa kutamba, amekuwa na msimu mzuri zaidi na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, msimu huu.



## HABARI MICHEZO



# CITY HATARINI KUPOTEZA NYOTA WAKE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City inaweza kupoteza wachezaji wake nyota ambao wameripotiwa kutaka kuondoka.

Winga Leroy Sane amekamilisha usajili wa kwenda kukipiga Bayern Munich ya Ujerumani huku kiungo, Kevin De Bryune naye akisubiri kuona rufani ya klabu hiyo dhidi ya marufuku ya kutoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya itatoka na uamuzi gani.

Pia kocha mkuu wa klabu hiyo, Pep Guardiola naye hajaweka wazi hatima yake ndani ya klabu hiyo kama ataongeza mkataba au ataondoka.

Kocha huyo aliyeiwezesha kubeba mataji kadhaa yakiwamo ya Ligi Kuu England, Carabao na FA, mkataba wake umebaki mwaka mmoja tu na hakuna mazungumzo mapya mpaka sasa.

Habari za ndani ya klabu hiyo zinadai kuwa Guardiola hana mpango wa kuendelea kuwapo Etihad baada ya msimu ujao kukiwa na sintofahamu kuhusu ushiriki wake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nafurahia kuwa sehemu ya mafanikio ndani ya klabu, tumepoteza msimu huu, lakini tunajipanga vyema kuwakabili Liverpool msimu ujao," alisema Guardiola alipoulizwa kuhusu mikakati yake ya baadaye.

"Nitafanya kwa uwezo wangu ili kuwa na mafanikio. Lakini, sitaki kufikiria mipango ya mbali zaidi. Kwa sasa nawaza tuna mechi ngumu mbele yetu."

City inajiandaa kuingia kwa kishindo kwenye soko kutokana na kauli ya De Bruyne, huku Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, akiwa majeruhi na Raheem Sterling akiwa bado hajasaini mkataba mpya huku Barcelona na Real Madrid zikitajwa kumwania.

# HAVERTZ ATOA MASHARTI UNITED, CHELSEA

**MUNICH, Ujerumani**

NYOTA wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz ameripotiwa atazipiga chini ofa za kutoka Manchester United na Chelsea kama hazitafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.


Havertz, anataka kucheza kwenye michuano ya Ulaya msimu ujao, hivyo jambo hilo ni mtego kwa timu za Chelsea na United zinazomsaka, kuhakikisha zinafanya kweli na kukamata tiketi hiyo.

Kwa sasa, timu hizo zipo kwenye nafasi ya nne na tano, Chelsea wakiwa juu kwa tofauti ya pointi tano, huku zikiwa zimebaki mechi saba Ligi Kuu England kufika tamati.

Kama timu zote zitafuzu kucheza michuano hiyo ya Ulaya msimu ujao, basi itakuwa kazi ya Havertz kuchagua kwenda Old Trafford au Stamford Bridge.

Havertz amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu, akifunga mabao 16 na pasi za mwisho tisa katika mechi 41 za michuano yote alizoitumikia Leverkusen.

Klabu kadhaa zimevutiwa na huduma yake zikiwamo Real Madrid na Bayern Munich pia na zimeonyesha dhamira ya kuhitaji kumsajili wakati dirisha la majira ya kiangazi litakapofunguliwa.



# SANCHO ATABIRIWA MAKUBWA UNITED

**LONDON, England**

GWIJI wa zamani wa Arsenal, Ian Wright anaamini kwamba, Manchester United imeanza kurejea kwenye kiwango chake cha zamani.

Amesema viwango vya juu vinavyoonyeshwa na mastaa wake Bruno Fernandes, Paul Pogba, Anthony Martial na Marcus Rashford vimewafanya wababe hao kuwa bora zaidi uwanjani.

Hata hivyo, Wright ambaye amecheza kwa mafanikio makubwa wakati huo Arsenal ikiwa chini ya Arsene Wenger, alisema kuna mtu mmoja ambaye United wanapaswa kumnasa ili kuwa watamu zaidi na kuwania mataji mbele ya Liverpool na Manchester City.

"Kwa sasa kila mtu anakunwa na ubora wa Fernandes, Pogba na Rashford uwanjani. Nadhani Manchester United wanarudi kwenye ule ubora wao kama wakati wa Ferguson (Sir Alex) na kushinda mataji. Lakini, wataongeza ushindani zaidi kama watamnasa Sancho (Jadon)," alisema Wright akinukuliwa na Sky Sport.

Alisema amekuwa akiifuatilia Man United namna inavyocheza na kubaini kuwapo na tofauti kubwa na sasa iko tayari kwa ushindani dhidi ya Liverpool na Manchester City kama itaongeza wachezaji wachache kwenye maeneo muhimu.

"Inashtua kwa kweli, angalia Fernandes na Pogba wanavyocheza pamoja ama Martial na Rashford na aina ya mabao wanayofunga uwanjani."

United ilishinda mchezo huo kwa mabao 2-1 ndani ya dakika 120 baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya 1-1.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG AZIDI KUIFIKIRISHA ARSENAL

●●●Kocha wake Arteta anaamini mshambuliaji huyo atabaki Emirates na anafuraha...

**LONDON, England**

KOCHA Mikel Arteta, anaamini nahodha, Pierre-Emerick Aubameyang atafunga tena mabao mengine 100 kwa Arsenal baada ya kufikisha magoli 50 kwenye Ligi Kuu England kwenye mechi iliyomalizika kwa ushindi dhidi ya Norwich.

The Gunners walikuwa katika kiwango bora katika mechi hiyo ambapo Aubameyang alifunga mabao mawili pamoja na Granit Xhaka aliyekuwa akicheza mechi yake ya kwanza msimu huu na baadaye Cedric Soares akakamilisha ushindi wa magoli 4-0.

Aubameyang alifunga goli la kwanza baada ya kuwahi mpira ulioanzishwa na golikipa wa Norwich, Tim Krul, ambalo lilimfanya afikishe mabao 50 kwenye Ligi Kuu England, akiwa amecheza mechi 79 na kumfanya kuwa mchezaji wa Arsenal aliyefunga idadi hiyo mapema.

Akizungumza baada ya ushindi wa mechi hiyo, Kocha wa Gunners, Arteta, alimpongeza Aubameyang na kumtaka aendelee kupambana kuhakikisha anafunga mabao zaidi kwenye michezo inayofuata.

"Mchezaji ambaye anaweza kufunga mabao mengi zaidi kila anapopata nafasi na akiwa ndani ya muda mfupo ameonyesha anajua na kuhusu umuhimu wake kwetu," Arteta alimwelezea mshambuliaji huyo.

"Wachezaji wanaweza kuonyesha tofauti wakati wowote wa mchezo ndani ya siku tatu kwenye mashindano mbalimbali. Huu ni mpango wa kiwango cha juu na amefanya hivyo akiwa na klabu tofauti.

"(Ninaamini ataendelea kufunga) anaweza kufikia mabao 100 lakini huwezi kujua. Mimi sio mtu wa miujiza.

" Kile ambacho amefikia leo kuwa mchezaji aliyefunga mabao 50 mapema zaidi ni historia kwenye klabu na inaonyesha wazi uwezo aliokuwa nao katika kufanya kazi yake kila siku."

Aubameyang amebakiza muda wa mwaka mmoja katika mkataba wake wa kubaki hapo Uwanja wa Emirates lakini, huku Arteta akisisitiza mazungumzo ambayo hakujumuishwa, anaamini nyota huyo raia wa Gabon atabaki klabuni hapo.

"Yuko tayari kubaki na sisi," aliongeza Arteta. "Anaonekana ana furaha ya kweli akiwa na sisi.

## KWA UFUPI

**GRIEZMANN KUONDOKA**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann (29), anapambana kuhakikisha klabu hiyo inampa ruhusa ya kujiunga na Arsenal au Inter Milan. ***(Express)***

**GUARDIOLA AMTAKA ALABA**

BEKI wa Versatile Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba (28), anatajwa kuwindwa na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola ambaye anataka kukijenga kikosi chake. ***(Guardian)***

**CITY YAACHANA NA SANCHO**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesitisha mpango wa kumrejesha kikosini kwake winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Sun)***

**ARSENAL YAMWOTA SILVA**

ARSENAL inaamini beki wake wa kati, David Luiz (33), atajaribu kumshawishi Mbrazil mwenzake, Thiago Silva (35), kujiunga na klabu hiyo baada ya kuondoka Paris St-Germain katika majira ya joto. ***(Le10 Sport, via Mail)***

**PARTEY KUTUA ARSENAL**

MABOSI wa Arsenal wamesema wanaongeza nguvu katika mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Atletico Madrid, Thomas Partey, lakini hawako tayari kulipa dau la pauni milioni 45, ambazo zimetajwa katika kipengele cha mkataba wake. ***(Athletic, via Mirror)***

**AURIER AKARIBIA SPURS**

BEKI wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Serge Aurier (27), anatajwa kuwindwa na klabu inayoshiriki Ligue 1, Monaco, ambayo inaamini itamsajili mchezaji huyo ifikapo majira ya joto. ***(Sky Sports)***

**CHRISTENSEN ANOGEWA CHELSEA**

BEKI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Denmark, Andreas Christensen, ambaye ana umri wa miaka 24, amesema hana nia ya kuondoka klabuni hapo na amefungua milango ya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya wa kubaki Stamford Bridge. ***(Goal.com)***

**MKHITARYAN KIMEELEWEKA**

KIUNGO wa Arsenal na Armenia, Henrikh Mkhitaryan (31), huenda akajiunga moja kwa moja na Roma baada ya mkataba wake wa mkopo na klabu hiyo ya Serie A kuongezwa. Hata hivyo inatajwa kuwa winga Mholanzi, Justin Kluivert (21), anakaribia kujiunga na Arsenal. ***(Mail)***

**MOURINHO AMJENGA NDOMBELE**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, amesema mchezaji aliyeweka rekodi ya kusajiliwa kwa gharama za juu katika klabu hiyo, Tanguy Ndombele (23), anaweza kuwa kwenye kiwango bora hapo Spurs, licha ya kiungo huyo Mfaransa kupata wakati mgumu katika msimu wake wa kwanza. ***(Guardian)***

**SPURS KUMTOA KYLE**

SPURS inatarajia kumtumia beki wake wa kulia, Kyle Walker-Peters (23), ambaye yuko kwa mkopo Southampton, kama sehemu ya mchakato wa usajili wa kiungo wa Saints, Pierre-Emile Hojbjerg, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Football London)***

**SALAH KUZEEKEA LIVERPOOL**

WINGA wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah (28), amesema anataka kubakia klabuni hapo kwa muda mrefu zaidi. ***(Bein Sports, via Express)***

**MESSI ATAKIWA ARGENTINA**

MAKAMU wa Rais wa Newell's Old Boys, Cristian D'Amico, anaamini mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi (33), atarejea katika klabu yake ya utotoni, baada ya kujiunga na vigogo hao wa Hispania akiwa na umri wa miaka 13. ***(TNT Sports, vial Goal)***

HABARI MICHEZO

# DOMAYO: SIKUDHAMIRIA KUMUUMIZA KAPOMBE

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa mabingwa watetezi wa Kombe la FA, Azam FC, Frank Domayo, amwomba msamaha beki wa pembeni wa Simba, Shomari Kapombe na kuongeza hakudhamiria kumuumiza nyota huyo.

Domayo alimkanyaga Kapombe sekunde chache kabla ya mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la FA kati ya Simba na Azam kumalizika, rafu iliyopelekea beki huyo kuondolewa uwanjani kwa machela.

Kitendo hicho cha Domayo cha kumkanyaga Kapombe wakati wakiwania mpira uliokuwa ukimilikiwa na Kapombe kiliamsha hasira kwa beki huyo aliyeonekana kuchukizwa pamoja na wachezaji wengine wa timu hiyo pamoja na kocha wa viungo, Adel Zrane.

Akizungumza gazeti hili jana, Domayo, alisema hakufanya kitendo hicho kwa makusudi kama ambavyo baadhi ya mashabiki walivyotafsiri isipokuwa tukio hilo lilitokea katika hali ya kawaida ya kuwania mpira.

"Namwomba radhi rafiki yangu Kapombe, sikuwa na dhamira ya kumuumiza, najua ameumia, lakini naomba nieleweke ni kitendo cha bahati mbaya," alisema Domayo.

Kiungo huyo wa zamani wa Yanga alisema ilikuwa ni 'presha' ya mchezo na tukio hilo lilikuwa la kugombania mpira ambao walikuwa wanaukimbiza wote.

"Nimeumia sana baada ya kuona Kapombe ameumia na namna tukio lenyewe lilivyochukuliwa na mashabiki pamoja na wadau wa mpira, sikufanya kwa makusudi," aliongeza Domayo.

Katika mchezo huo, Simba iliwavua ubingwa wa michuano hiyo, Azam baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 na kusonga mbele katika michuano hiyo inayotarajiwa kuendelea tena kati ya Julai 11 na 12, mwaka huu.



Wachezaji wa Sahare All Stars wakishangilia baada ya kuiondoa Ndanda FC kwa penalti 4-3 katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga juzi. **PICHA : OSCAR KASIMIRI**

# Mlandege yatinga kileleni Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MLANDEGE imefanikiwa kutinga kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupata ushindi bao 1-0 dhidi ya Zimamoto katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau B visiwani hapa juzi.

Kwa matokeo hayo, Mlandege ilifikisha pointi 47 huku nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo ikishikiliwa na KMKM yenye alama 46 wakati JKU wenye pointi 43 wako katika nafasi ya tatu.

Mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Gombani, ilikuwa ni kati ya Selem View iliyolazimishwa sare ya bila kufungana na Mafunzo wakati wenyeji Jamhuri walichapwa mabao 2-0 na Polisi.

Katika Uwanja wa Mau A Maafande wa Kipanga na JKU walishindwa kutambiana baada ya kutoka suluhu.

Mwenyekiti wa Mlandege, Mbaraka Himid, alisema ushindi walioupata umetokana na jitihada binafsi za wachezaji kwa sababu timu yao haikufanya mazoezi kama klabu nyingine zilivyojiandaa kuendelea na ligi hiyo.

Himid alisema wachezaji walicheza kwa hamasa kubwa licha ya kutokuwa na mashabiki lakini walijitahidi kuonyesha kandanda safi katika dakika zote za mchezo na kuufanya mchezo huo kuwa mgumu kwa wapinzani wao kuliko ilivyotegemewa.

Aliongeza lengo lao la kunyakuwa ubingwa wa ligi hiyo halijafutika na watahakikisha michezo iliyobaki wanafanya vizuri ili kuwapa furaha mashabiki wao ambao wanausubiri ubingwa huo kwa hamu kubwa.

## Sahare yatamba itacheza fainali

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA kwa kuichapa Ndanda FC kwa penalti 4-3, Sahare All Stars imetamba itacheza fainali ya michuano hiyo itakayofanyika kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Sumbawanga.

Sahare All Stars, ilifika hatua ya matuta baada ya kumaliza dakika 90 wakiwa na sare ya bao 1-1 katika mechi iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Ofisa Habari wa Sahare All Stars, Shali Stambuli, alisema ushindi wao ni kazi nzuri ya viongozi, mashabiki na wachezaji wa timu hiyo ambao waliungana na kuamua timu yao ifanye vizuri kwenye michuano.

Sahare All Stars inaweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza ya Daraja la Kwanza Tanzania Bara kufika hatua hiyo ya nusu fainali kwenye michuano hiyo.

Wakati Sahare ilishangilia ushindi, majonzi makubwa yamekwenda kwa Ndanda ambayo ilitolewa kwenye hatua hiyo, huku viongozi wakisema wachezaji wao waliidharau mechi.

"Timu ilikuwa chini kimorali, hatukucheza kwenye hali ya kawaida, lakini nadhani tuliwadharau," alisema Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Selemani Kachele.

Alisema wanakubali kushindwa na sasa wanaelekeza nguvu zao katika mechi za Ligi Kuu Bara zilizobaki.

## Dereva Shusha Mizigo yakamilika

**Na Sabato Kasika**

RAPA wa siku nyingi wa muziki wa dansi, Greyson Semsekwa, ameibuka na rapu mpya iitwayo 'Dereva Shusha Mizigo' ambayo itakuwa kwenye albamu mpya inayoandaliwa na bendi ya Waluguru Original ya mkoani Morogoro, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Semsekwa alisema, rapu hiyo ni utambulisho wa ujio wake mpya baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu tangu alipoachana na bendi kongwe ya African Stars 'Twanga Pepeta'.

"Kwa sasa maskani yangu yako mjini Morogoro nikiwa na bendi ya Waluguru Original na nimeshusha rapu ya 'Dereva Shusha Mizigo', ambayo itakuwa kwenye albamu mpya tunayoendelea kuiandaa," alisema Semsekwa.

Aliongeza bendi hiyo kwa sasa imekamilisha nyimbo sita ambazo ni 'Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe, ambazo zinapamhwa na rapu yake.

Alifafanua kuwa muziki wa dansi kwa sasa una mashabiki karibu kila kona ya nchi, hivyo haoni kwa sababu ya 'kujichimbia' jijini Dar es Salaam wakati kuna fursa ambayo ameipata Morogoro.

Semsekwa aliibuliwa na bendi ya Extra Bongo mwanzoni mwa mwaka 2000 na kujizolea umaarufu katika muziki wa dansi kwa rapu zake mbalimbali ikiwamo ya 'Kichaa Kapewa Rungu, Usijaribu Kupita Mbele Yake'.

Michezo
Ijumaa Julai 3, 2020
Nipashe



Aubameyang azidi kuifikirisha Arsenal

HABARI UK 22




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Pavel Slavkov (kulia), akimkabidhi zawadi ya hundi ya Sh. milioni 100, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha kama bonasi baada ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20. Kushoto ni Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA YAFURAHI KUIFUATA YANGA

●●●Sven afunguka bao la Morrison linamnyima usingizi licha kutetea ubingwa Ligi Kuu...

**Na Faustine Feliciane**

TUTAONA! Baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck amesema amefurahi kupata nafasi nyingine ya kukutana na watani zao, Yanga ndani ya msimu huu.

Simba ambao tayari ni mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imesonga mbele katika michuano hiyo kwa kuwafunga Azam FC mabao 2-0 na kuwavua ubingwa wa michuano hiyo waliokuwa wanaushikilia.

Mechi za nusu fainali ya mashindano hayo zitachezwa Julai 12, mwaka huu kwa Sahare All Stars kuikabili Namungo FC, huku Simba ikivaana na Yanga siku hiyo hiyo kuanzia saa 11: 00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Sven aliliambia gazeti hili kitendo cha kupoteza mchezo wao wa marudiano wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga ndio kimechangia 'atamani' kukutana na timu hiyo hivi karibuni.

"Kufungwa kwenye ligi kulitumiza sana, nashukuru matokeo haya dhidi ya Azam, sasa yanatupa nafasi ya kulipiza kisasi kwa Yanga kwenye hatua muhimu ya nusu fainali ya FA," alisema Sven na kuongeza;

"Utakuwa mchezo mzuri sana, nimefurahi tumesonga mbele lakini nimefurahi zaidi kwa kuwa tutakutana na Yanga na kupata nafasi ya kulipiza kisasi," alisema kocha huyo.

Mbelgiji huyo alisema licha ya kubakiwa na michezo mingine ya Ligi Kuu, lakini wanaanza mikakati ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo dhidi ya Yanga.

Kocha huyo alichukizwa na rafu iliyofanywa na kiungo wa Azam, Frank Domayo dhidi ya beki wake, Shomary Kapombe na kusema si cha kufumbiwa macho.

"Ninakitafsiri kama kitendo cha makusudi cha kumuumiza beki huyo ambaye ametoka majeruhi hivi karibuni. Kwangu mimi mwamuzi alistahili kumwonyesha kadi, lakini pengine hakuona, halikuwa tukio zuri na naona ni rafu ya makusudi," Sven alisema.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wanasubiri majibu ya vipimo vya Kapombe pamoja na Kennedy Juma, ambaye naye aliumia katika mchezo huo.

"Kwa sasa siwezi kusema lolote kwa sababu asubuhi hii (jana), Kapombe na Kennedy wamepelekwa hospitali, baada ya kurejea na vipimo vyao ndio tunaweza kusema lolote," alisema Rweyemamu.

Shukrani mabao yaliyofungwa na mshambuliaji na nahodha, John Bocco na kiungo Mzambia, Clatous Chama.

Wakati huo huo, hatima ya sakata la kiungo mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison dhidi ya klabu yake ambalo limetinga katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inatarajia kujulikana leo, imefahamika.

TFF ilimwita Mghana huyo juzi kwa mahojiano maalumu baada ya kuwapo kwa sintofahamu na klabu yake kuhusiana na mkataba mpya wa miaka miwili aliousaini mapema Machi, mwaka huu.

Habari nyingine zilizopatikana jijini zinaeleza pia kiungo huyo alicheza mechi mbili za awali bila ya kuwa na mkataba na Yanga.

## AZAM YAWAOTA MKUDE, CHAMA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amewataja viungo watatu wa Simba ambao ni pamoja na Jonas Mkude, Clatous Chama na Gerson Fraga ndio 'walivurunga' mipango yao ya ushindi katika mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi.

Simba ilishinda mabao 2-0 na kuwavua Azam FC ubingwa wa mashindano hayo ambayo bingwa wake atapata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Bahati, alisema Simba walikuwa bora katika safu ya kiungo na nyota hao walikuwa kikwazo kikubwa kwa timu yao.

Bahati alisema Simba walicheza katika kiwango cha juu katika mchezo huo na kwa kiasi kikubwa safu ya ulinzi ya Azam ilishindwa kuhimili ushindani.

"Simba walikuwa bora katikati, ndio sehemu imecheza mpira mwingi sana, hadi kuharibu mipango yetu na kushindwa kufanya vizuri katika mchezo huo wa robo fainali," alisema Bahati.

Alisema walijiandaa na mechi vizuri, huku wakiwaonyesha wachezaji wao ubora na mapungufu ya Simba ili kuweza kuyatumia na kupata matokeo mazuri katika mchezo wao huo robo fainali.

"Tuliandaa mipango vizuri lakini ubora wa viungo wa Simba, waliharibu mipango yetu, yale ambayo tuliyapanga hatukuyaona kabisa pale uwanjani kwa wachezaji wetu, walistahili ushindi," Bahati alisema.

Aliongeza baada ya kuondolewa kwenye michuano hiyo, sasa wanajipanga kuhakikisha wanalinda heshima kwa kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati huo huo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, amesema kiungo wa Azam FC, Frank Domayo amemwomba radhi beki wa Simba, Shomari Kapombe kutokana na kitendo cha kumchezea rafu katika mechi hiyo ya juzi.

Manara alisema pia Domayo amempigia simu nahodha wa Simba, John Bocco, ili amwombee radhi kwa wachzeaji wote wa Wekundu wa Msimbazi kutokana na tukio hilo na kuongeza hakuwa na dhamira mbaya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042